Leo yetu ndiyo kesho yetu

# Uelekeo



## Zuma asimamishwa uanachama wa ANC

Uk. 19

| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00049 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Januari 31 - Februari 6, 2024 |

# Samia aanisha mipango kamambe sekta ya uvuvi

- **Kujenga Bandari mbili za kisasa za uvuvi kubwa EA**




Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akielekeza jambo kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdalla Ulega, alipokuwa akielezea aina mbalimbali ya samaki wanaopatikana katika Ziwa Victoria baada ya uzinduzi wa boti ya kisasa na vizimba vya kufugia samaki jijini Mwanza jana.

## Waendesha bodaboda watishia kugoma



Uk. 5

## Mambo 5 ya kujua kuhusu nimonia



Uk. 8

## 'Wawekezaji wanaohitaji ardhi karibu Kigamboni'

Uk. 3

## Rushwa ya ngono vyuoni bado hali si shwari

**Na Godfrey Sanga**

NAIBU Waziri wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, amesema kati ya mwaka 2020 hadi mwaka jana, taarifa 11 za malalamiko ya vitendo vya rushwa ya ngono vyuoni zilipokelewa na majalada tisa ya uchunguzi, yameanzishwa.

Uk.4



## Madaktari bingwa China watua MOI

Uk. 3

Tanzania na China zimekuwa katika uhusiano kwa zaidi ya miaka 60 sasa...ujio wa madaktari hawa ni muendelezo wa ushirikiano huo,

## Paul Makonda anavyosaidia kutekeleza Ilani

Uk. 12

Ubingwa wangu unatokana na uwezo wa Mungu na nafasi aliyonipa Mwenyekiti na Rais wetu, Dk. Samia.



## Tarura yarejesha miundombinu iliyoharibiwa na mafuriko Dar

# Jaji awafunda watoto walioko mahabusu

**Na Mwandishi Wetu, Mbeya**

JAJI Mfawidhi Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Mbeya, Dunstan Ndunguru, amewataka watoto walio katika mahabusu, kubadili mienendo yao na kutokinzana na sheria wawapo uraiani.

Akiwaweka sawa watoto hao, Jaji Ndunguru alisema wanatakiwa kuwa watulivu na kuacha kujiona kama wametengwa.

Alisema ni vema wakajiweka sawa ili baadaye wawe watu wema na wenye mafanikio.

"Ninyi bado watoto na umri wenu bado mdogo, hamtakiwi kujihusisha katika kutenda makosa ya namna yoyote, mnatakiwa kujiepusha na makundi yasiyofaa ambayo yanawasababishia watoto kukinzana na sheria ya nchi yetu," alisema.

Alisema hayo yeye pamoja na ujumbe wake walipotembelea mahabusu ya watoto mkoani hapa ikiwa na lengo la kutekeleza shughuli mbalimbali zilizoambatana na maadhimisho ya Wiki ya Sheria na kilele cha siku ya sheria nchini.

Katika ziara hiyo, Jaji Ndunguru aliambatana na Jaji Victoria Nongwa, wa Mahakama Kuu ya Kanda hiyo, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya Mbeya, Teddy Mlimba, Mahakimu, Wakili wa Serikali, Wakili wa kujitegemea na wadau wengine wa Mahakama.



Jaji Mfawishi Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Mbeya, Dunstan Ndunguru.

# Magu yajipanga kudhibiti vifo wajawazito

**Na Mwandishi Wetu, Mwanza**

HOSPITALI ya Wilaya ya Magu mkoani Mwanza, imeweka lengo la kudhibiti vifo vitokanavyo na uzazi kwa kuhakikisha hakuna wajawazito wanaojifungulia nyumbani.

Takwimu za wilaya hiyo zilionesha kwa kipindi cha miaka mitatu vilitokea vifo 11 vitokanavyo na kujifungua, huku mwaka 2021 kati ya waliojifungua 18,468 vifo vilikuwa vinne, mwaka 2022 vinne kati 19,290 waliojifungua na 2023 vifo vitatu kati ya 19,721.

Kaimu Mganga Mkuu hospitali hiyo, Eusebius Chanjali, aliyasema hayo wilayani hapo mbele ya maofisa kutoka Wizara ya Afya, Tamisemi na waandishi wa habari, waliokuwa kwenye ziara ya kubaini mafanikio ya Mfuko wa Afya wa pamoja nchini (Health Basket Fund-HBF) kwa kipindi hicho.

"Wanaojifungua hospitalini hapa, ni wastani wa 300 kwa mwezi. Tumejihakikishia hakuna mama anayejifungulia nyumbani ili kuondoa kabisa vifo vya kinamama. Idadi ya vifo imepungua kutoka digiti mbili mwaka 2019 ambavyo vilikuwa zaidi ya 20, sasa vifo ni digiti moja," alisema.



# Rukwa yapania kunyakua Tuzo ya Kilimo msimu huu

**Na Mwandishi Wetu**

MKOA wa Rukwa umejipanga kuupiku Mkoa wa Ruvuma kwa uzalishaji wa mazao ya nafaka nchini kwa matarajio ya kuvuna tani zaidi ya 1, 654,840 za nafaka kwa msimu huu wa kilimo.


Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Makongoro Nyerere, akitoa taarifa kwa waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa shughuli za maendeleo mkoani humo juzi, alisema hali ya mazao mashambani kwa msimu huu wa kilimo ni nzuri.

Taarifa hiyo ilitolewa pia mbele ya watendaji wa mkoa, wakuu wa wilaya na wakurugenzi watendaji pia, kufuatia mikutano inayopangwa na kuratibiwa na Ofisi ya Msemaji wa Mkuu wa Serikali na Idara ya Habari (Maelezo) kwa kila mkoa kupata fursa ya kueleza utekelezaji wa shughuli za miradi ya maendeleo.

Katika sherehe za Nananane zilizofanyika jijini Mbeya mwaka jana, Rais Dk. Samia alitoa tuzo kwa Mkoa wa Ruvuma kuwa wa kwanza kwa uzalishaji wa mazao ya nafaka nchini, (mara tano mfululizo) ikifuatiwa na Mkoa wa Rukwa.

Makongoro alisema kutokana na hali ya mazao mashambani kuwa nzuri, wanatarajia kuupiku Mkoa wa Ruvuma au kuendelea kushikilia namba mbili.

Alisema uamuzi wa Rais Dk. Samia kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima, umesaidia mno kuongeza uzalishaji wa mazao.



Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Makongoro Nyerere.

# Laigwanani `wawapiga jeki' waathirika wa moto

**Na Mwandishi Wetu, Arusha**

WAZEE wa kimila wa jamii ya Kimasai maarufu kama Laigwanani katika Kata ya Engikaret Wilaya ya Longido, mkoani Arusha, wametoa msaada wa vyakula, nguo, maji na vyombo vya kupikia kwa familia ya watu 11 waliokumbwa na mkasa wa nyumba zao kuchomwa moto.

Familia hizo zilikumbwa na mkasa huo mara mbili, Desemba 29, mwaka jana na Januari 26, mwaka huu.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, alikiri kutokea kwa matukio hayo na kueleza kuwa hatua zimeanza kuchukuliwa ikiwemo ya kuwasaka watu waliofanya ukatili huo.

Mongella alisema timu ya watalaamu ilishakwenda eneo la tukio na wanasubiri kujua tathmini ya nyumba zilizochomwa moto huku serikali ikiendelea na uchunguzi kuwabaini waliofanya kitendo hicho.

''Ni kweli tukio hilo lilitokea na siyo kwamba serikali imekaa kimya, iko kazini inafanyia kazi na wote waliohusika watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria,'' alisema Mongella.

Awali, akizungumza kwa niaba ya wazee wa kimila, Laigwanani Elia Lukumay, alisema wameamua kutoa msaada kwa familia hizo kwa kuwa serikali ilikaa kimya bila ya kuwasaidia waliochomewa nyumba kwani hakuna hatua zilizochukuliwa dhidi yao.

Lukumay alisema maboma matatu na nyumba 11, zilichomwa moto, mifugo ikiwemo mbuzi wadogo sita na kuku 18. Matukio yote mawili yalifanyika mchana majira ya saa saba na tisa alasiri.

Msaada wa vitu vilivyotolewa na wazee hao ni magunia 10 ya mahindi, madumu saba ya maji, mafuta ya kupikia madumu matatu na vyombo vya kupikia.

Naye mmoja wa Waathirika, Lucy Jacob, kwa niaba ya wenzake, aliwashukuru Laigwanani kwa msaada huo kwani wako katika maisha magumu kwa sasa na walimuomba Mbunge wa Jimbo hilo, Dk. Stephen Kiruswa, kuwakumbuka na ikibidi kuwasaidia kwa namna moja ama nyingine.



# Madaktari bingwa wa China watua MOI

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Tiba ya Mifupa na Ubongo Muhimbili (MOI), imewapokea madaktari bingwa wa mifupa na ubongo kutoka China watakaohudumu kwa kipindi cha miaka miwili ikiwa ni muendelezo wa ushirikiano baina ya Tanzania na China.

Akizungumza wakati wa hafla fupi ya kuwapokea madaktari hao juzi kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji, Mkurugenzi wa Upasuaji wa Ubongo wa MOI, Dk. Lemeri Mchome, aliishukuru Serikali ya China na kuongeza ujio wa madaktari hao utaongeza ujuzi na umahiri kwa madaktari wazawa.

"Wenzetu China wamepiga hatua katika tiba za mifupa, ubongo na mishipa ya fahamu, hivyo, uwepo wao hapa utasaidia kuwajengea uwezo kwa madaktari wetu, ninaamini walivyotukuta sivyo ndivyo watakavyotuacha, umahiri wetu utakuwa umepanda," alisema.

Kwa upande wake, mwenyeji wa madaktari hao, Dk. Liggy Vumilia, kutoka Wizara ya Afya alisema madaktari hao 11 watakuwapo nchini kwa miaka miwili wakitoa huduma MOI, Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya.

"Tanzania na China zimekuwa katika uhusiano kwa zaidi ya miaka 60 sasa...ujio wa madaktari hawa ni muendelezo wa ushirikiano huo, wito wangu kwenu ni kuhakikisha mnawatumia vyema madaktari hawa ili tupate ujuzi walio nao, ni imani ya wizara kuwa huduma zetu zitaboreshwa kwa kuwatumia vizuri madaktari hawa," alisema.

Mratibu wa Mafunzo na Utafiti wa MOI, Dk. Joel Bwemelo, alisema ujio wa madaktari hao bingwa unalenga kubadilishana uzoefu wa kutoa tiba kwa ufanisi na hivyo kuboresha huduma kwa wagonjwa.

"Tumepokea madaktari bingwa watatu, mmoja wa usingizi, mwingine wa mifupa na wa tatu ni wa ubongo, wawili watakuwapo hapa kwa mwezi mmoja na nusu kabla ya kwenda Hospitali ya Rufaa Mbeya, na huyu mmoja atakuwa MOI kwa miaka yote miwili.

Kiongozi wa madaktari hao, Dk. Cheny Jiyong, alishukuru MOI kwa mapokezi na kuahidi kutoa ushirkiano wa dhati katika kutekeleza majukumu yao.




# `Wawekezaji wanaohitaji ardhi karibu Kigamboni'

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

SERIKALI inawakaribisha wakwezaji wa ndani na nje ya nchi kuwasilisha maombi ya uhitaji wa ardhi ya uwekezaji katika ekari 1,000 eneo la Pembamnazi, Wilaya ya Kigamboni mkoani Dar es Salaam.

Waziri wa Nyumba, Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, alitoa kauli hiyo jana katika Mkutano wa 14, kikao cha kwanza cha Bunge jijini Dodoma wakati akijibu swali la Mbunge wa Kigamboni, Dk. Faustine Ndugulile, kuhusu matumizi ya eneo hilo.

Alisema Serikali kupitia wizara yake, inatafuta wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kuwapatia kiwango chochote watakachohitaji.

"Serikali inatafuta wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza katika eneo la ekari 1,000 zilizopo Pembamnazi, Wilaya ya Kigamboni, lengo la Rais Samia kutenga eneo hilo ni kuongeza uwekezaji hapa nchini," alisema Waziri Silaa.

Aidha, alifafanua kwamba wawekezaji wawasilishe maombi katika Ofisi ya Ardhi jijini Dar es Salaam pamoja na kwamba eneo hilo lilipimwa miaka mitano iliyopita, lakini tayari wameanza kupokea maombi hayo.



Waziri wa Nyumba, Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa.

# Wastaafu wamuangukia Rais Dk. Samia nyongeza ya pensheni

**Na Lauden Mwambona, Mbeya**

WASTAAFU wanaopata pensheni kila mwezi nchini, wamemuomba Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kuiagiza mifuko ya hifadhi ya jamii (PSSSF na NSSF), kurudisha utaratibu wa kutoa nyongeza ya pensheni kila baada ya miaka mtatu au mitano kwa wanaopokea kila mwezi ili wakabiliane na changamoto za makali ya maisha.

Wamesema miaka ya 1990, mifuko ya hifadhi ya jamii, ilikuwa ikiongeza kiasi cha fedha kila baada ya miaka mitatu, lakini tangu miaka ya 2015, haifanyi hivyo.

Wamesema karibu miaka 10 sasa mifuko ya hifadhi ya jamii haijaongeza posho wanayopokea wastaafu na kwamba wamedumu kwenye viwango vya zamani bila nyongeza licha ya wafanyakazi kuongezwa mishahara.

"Mimi nilianza kupata pensheni ya Sh. 187,400 mwaka 2016 , mpaka sasa bado napata kiwango hicho hicho," alisema mstaafu Mwanahamisi Abdallah, mnkazi wa jijini Mbeya.

Mwanahamisi amemuomba Rais Dk. Samia kuwaongeza wastaafu kiasi chochote ili waweze kukabiliana na changamoto zinazowakabili baada ya kulitumikia taifa kwa miaka mingi na uadilifu.

Naye mstaafu Adamu Mwakihaba, alisema hajawahi kuona nyongeza kwenye pensheni yake tangu alipoanza kupokea 2014 na kwamba wastaafu wamesahauliwa moja kwa moja, jambo ambalo halijengi afya.

Hoja kama hizo pia zilitolewa na wastaafu Ngetule Mwashilindi, mkazi wa wa Vwawa na Thobias Mwasha, mkazi wa Mlowo mkoani Songwe ambao pia wamemuomba Rais Dk. Samia kuliangalia suala hilo kwa jicho la huruma.

Ofisa wa PSSSF ngazi ya Mkoa wa Mbeya alipoulizwa kuhusu suala hilo, alisema ni la kitaifa na kwamba ni vigumu kulizungumzia.

Hali kadhalika, maofisa wa NSSF Mikoa ya Mbeya na Songwe, walitoa kauli kama hiyo.

Hata hivyo, uchunguzi wa mwandishi wa habari hii umebaini kuwa , kumekuwepo na aadhi ya wanachama kujitoa kwenye mifuko hiyo hata kabla ya wakati na kudai kulipwa mafao yao, jambo linaloweza kuzorotesha afya ya mifuko hiyo.

Mathalani, taarifa za mmoja wa mifuko hiyo imeonyesha kwa kipindi cha miezi mitatu kati ya Oktoba na Desemba, mwaka jana, takribani wanachama 25,000 wameomba mafao kwa kujitoa kabla ya muda wa kustaafu na kuufanya mfuko huo kuwalipa zaidi ya Sh. bilioni 34.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

# Samia aanisha mipango kamambe sekta ya uvuvi

## ■ Kujenga Bandari mbili za kisasa za uvuvi kubwa EA

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, ameanika mipango madhubiti ya kukuza sekta ya uvuvi akisema serikali anayoingoza itajenga bandari mbili za kisasa za uvuvi ambazo zitakuwa kubwa kuliko zote katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Alisema serikali imejipanga kikamilifu kuchochea ukuaji wa sekta ya uvuvi kupitia mpango na programu mbalimbali ili kuongeza mchango wa sekta hiyo katika Pato la Taifa.

Aliyasema hayo jijini Mwanza jana baada ya kukabidhi vizimba vya ufugaji samaki na boti 160 za uvuvi 160 za kisasa kwa vikundi vya vijana na binafsi wa Ukanda wa Ziwa.

"Miongoni mwa mipango hiyo, ni utekelezaji wa mradi wa kielelezo ikiwemo ununuzi wa meli ya uvuvi katika bahari kuu, ujenzi wa bandari za uvuvi katika maeneo ya Kilwa Masoko na Bagamoyo…kwa hiyo, tunajipanga hivyo, Kilwa tayari tumeanza na Bagamoyo hatuna muda tutaanza," alisema.

Alitaja miradi mingine kuwa ni ujenzi wa masoko ya samaki ya kisasa, ambapo soko moja litajengwa Nyamagana jijini Mwanza na ujenzi wa mialo ya kupokelea samaki na miundombinu ya kuhifadhia mazao ya uvuvi ili kupunguza upotevu baada ya kuvuna.

Vilevile, alisema serikali itaimarisha maeneo yanayofaa ya ufugaji wa samaki kwa kutumia vizimba katika Maziwa Makuu ya Tanganyika na Nyasa.

Mpango mwingine utakaotekelezwa ni ujenzi wa vituo vya kuendeleza ukuzaji wa viumbe maji na mashamba darasa ya ufugaji wa samaki.

Rais Dk. Samia alitaja mpango wa kuwawezesha vijana na wanawake kupitia fursa zinazopatikana katika sekta ya uvuvi inayojulikana kama 'Jenga kesho iliyo bora' BBT katika mifugo na uvuvi.



Alisema kwa mfano, katika mwaka 2022/23, vijana 200 wameshapatiwa mafunzo maalum kupitia mradi huo kwa ajili ya kuanzisha biashara na kampuni zitakazotumia raslimali za uvuvi na ukuzaji viumbe maji.

Aidha, alisema katika mwaka 20923/24, vijana wengine 300 wameshachaguliwa kujiunga na mafunzo hayo na wahitimu watapatiwa mikopo ya zana kama walivyopatiwa hao.

**Atoa maagizo kwa Mwanza**

Katika hatua nyingine, Rais Dk. Samia ameutaka uongozi wa Mkoa wa Mwanza kuhakikisha wanatumia Uwanja wa Ndege wa Mwanza kusafirisha mazao ya uvuvi.

"Najua haipendezi uwanja upo hapa, mazao yanavunwa hapa, yakasafirishwa kupitia uwanja wa ndege wa nchi nyingine…haipendezi hata kidogo," alisema.

Hata hvyo, alisema alitoa agizo kwa Mkuu wa Mkoa huo kumtaka pamoja mambo mengine, kufuatilia maboresho ya uwanja wa ndege kwa kuweka jengo jipya la abiria na jengo lenye miundombinu ya kuhifadhia samaki.

"Sasa nimeambiwa kwamba ujenzi huo `cold room' umeshaanza na unaendelea," alisema.

Kuhusu upatikanaji wa umeme wa uhakika katika viwanda vya kusindika samaki na vingine, alisema serikali itatatua changamoto hiyo na kwamba tatizo hilo linaendelea kupatiwa ufumbuzi.

Akizungumzia soko la mazao ya uvuvi, aliwataka wanaofanya kazi ya uvuvi, ukuzaji wa viumbe maji na wachakataji wa mazao ya uvuvi, kufanya kazi kwa nguvu kwa sababu soko la mazao ya samaki ni kubwa duniani.

Kuhusu wanufaika wa boti, aliwataka kurejesha mikopo kama walivyoingia mkataba ili wavuvi wengine nao wanufaike.

"Tunachokifanya leo hapa, ni sehemu tu ya mpango wa serikali wa kuwafikia wavuvi wengi zaidi kupitia vikundi vyao au mtu mmoja mmoja atakayeonesha ana uwezo zaidi," alisema na kuongeza:

"Tutaendelea kufanya hivyo kwa awamu kama ambavyo tulianza kule Kilwa na sasa Mwanza na tutaenda maeneo mengine ya pwani na watarudi tena hapa na tutakwenda Kigoma huko Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa, tutakwenda kuwaona wavuvi wote katika maeneo hayo."

Aliwataka wanufaika wa vifaa hivyo, kuongeza bidii na maarifa zaidi na kuzingatia ubora wa afya ya walaji.

"Lazima tuhakikishe afya ya walaji inazingatiwa na pia tusijiharibie katika masoko ya bidhaa hizo nje ya nchi au kimataifa," alisema.

Aidha, alisema uendelevu wa mradi huo kwa kiasi kikubwa unategemea uaminifu wa kurejesha mikopo ili wengine nao wanufaike.

"Najua kabla ya kupewa mikopo, mliwekwa kitako mkaelezwa kwamba huu ni mkopo na vizuri kwamba ni mkopo usio na riba siyo mkopo kama kausha damu, mfanye kazi kwa bidii kurejesha mikopo hiyo," alisema.

# Rushwa ya ngono vyuoni bado kizungumkuti

**Inatoka uk. 1**

Amesema kati ya majalada hayo, mawili yamefungwa baada ya kukosekana kwa ushahidi.

Ridhiwani aliyasema hayo Bungeni jijini Dodoma jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalumu, Amina Daud Hassan.

Mbunge huyo alitaka kufahamu kama serikali inatambua uwepo wa rushwa ya ngono kwa wanafunzi katika vyuo hapa nchini na hatua zilizochukuliwa.

Waziri Ridhiwani alisema jalada moja kati ya 11, limepata kibali cha kumfikisha mtuhumiwa mahakamani, majalada mawili yamependekezwa watuhumiwa wake wachukuliwe hatua za kinidhamu, jalada moja kesi imeshindwa mahakamani na majalada manne bado yanaendelea na uchunguzi.



**NAIBU Waziri wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete**

# Kamati ya Bunge Kilimo yatua mashamba ya miwa

**Na Mwandishi Wetu**

WAJUMBE wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, wametembelea mashamba ya miwa ya Mkulazi (Wilaya ya Kilosa) na Mtibwa (Wilaya ya Mvomero) sambamba na viwanda vinavyozalisha bidhaa hiyo ili kujionea hali halisi.

Ziara hiyo ilikuwa mahsusi kufuatilia uzalishaji wa sukari kwenye viwanda hivyo katika kipindi hiki cha mvua za El-Nino zinazoendelea nchini.

Wajumbe wa Kamati walijionea uharibifu mkubwa wa miundombinu uliosababishwa na mvua na kuzorotesha uzalishaji wa sukari na kupata fursa ya kuishauri serikali.

# Tarura yarejesha miundombinu iliyoharibiwa na mafuriko Dar

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA Barabara za Vijijini na Mijini (Tarura), imesema imefanikiwa kurejesha mawasiliano ya miundombinu katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Dar es Salaam na kufanya wananchi kuendelea na shughuli zao za uzalishaji wa kiuchumi na kijamii.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Meneja wa Tarura Mkoa wa Dar es Salaam, Mhandisi Geofrey Mkinga, wakati wa ukaguzi wa miundombinu katika Wilaya ya Kinondoni, Temeke na Ubungo.

Alisema Tarura inajipanga kukabiliana na uharibifu uliojitokeza na kutekeleza agizo la Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, la kuhakikisha mawasiliano yanarejeshwa na kwamba hakuna shughuli zitakazokwama na kuongezeka kwa gharama za usafiri kutokana na kukosekana kwa mawasiliano.

"Sisi kama Tarura, tangu Januari, mwaka huu, tunafanya kazi kwa kasi usiku na mchana na tutaendelea kuhakikisha shughuli za kiuchumi na kijamii zinarejea kama awali kwa wakazi wote wa Jiji hili la Dar es Salaam," alisema.

Aidha, alisema mvua nyingi zilizonyesha hivi karibuni, zilileta madhara makubwa kwa sababu ya ardhi kujaa maji na kusababisha barabara nyingi kuathirikia yakiwamo madaraja.

"Madaraja mengi hayajaathirika, lakini maingilio ya daraja ambayo sehemu ya tuta lake zimesombwa na maji, udongo ulijaa maji hivyo ilikuwa rahisi kuondoka kila maji yalipokuwa yamezidi kwenye madaraja yetu mengi," alisema Mhandisi Mkinga.

Mhandisi Mkinga alitaja madaraja yaliyoathiriwa kuwa ni daraja la Ally Hushumu, Mbopo, Madale, Msumi, Tanganyika, Majengo, Bwege pamoja na daraja la Msumi (Kivule).

Alisema madaraja yaliyoathirika kabisa na hivyo kutakiwa kujengwa upya hali ya hewa itakapotulia ni daraja la Msumi-Kivule (Ilala) ambalo limewekwa kivuko cha watembea kwa miguu pamoja na daraja la Msumi (Madale - Kinondoni) ambalo watatengeneza kivuko cha watembea kwa miguu kwani daraja hilo limeharibika zaidi na haliwezi kutengenezwa kwa haraka.

Aidha, Mhandisi Mkinga alieleza kuwa tayari ujenzi mpya wa daraja hilo pamoja na barabara ya Mbezi Msumi – Madale Kilomita 8.5, utafanyika chini ya Mradi wa DMDP 2 ambao unatarajia kuanza Mei, mwaka huu.

# Waendesha bodaboda watishia kugoma

**Na Mwandishi Wetu, Ruangwa**

BAADHI ya waendesha pikipiki maarufu kama bodaboda katika Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi, wametishia kugoma kutoa huduma hiyo kutokana na wimbi kubwa la wizi wa vyombo hivyo vya moto.

Maedereva hao wamesema watachukua hatua hiyo iwapo vyombo vya ulinzi na usalama, havitawabaini wezi hao na kuwachukulia hatua za kisheria kwani ndani ya wiki nane tu, jumla ya pikipiki nane zimeporwa na watu wasiofahamika.

Walisema uporaji huo wa pikipiki, umezua wasiwasi mkubwa miongoni mwa wamiliki na Waendesha bodaboda wa wilayani Ruangwa na vitongoji vyake.

Wakizungumza na gazeti Uelekeo katika vijiwe vya vituo vya mabasi katika uwanja wa Shule ya Msingi Likangara upande wa Mnada wa nguo, eneo la Kongo na Kwa D katikati ya mji, baadhi ya waathirika walisema, tangu uporaji huo uanze, hakuna mwizi aliyekamatwa.

"Kwa sasa, hakuna dereva wa bodoboda anayekubali kupakia abiria asiyemjua

kwenda nje ya mji. Hatua hii inatusababishia kupata kipato kidogo kila siku," alililalamika dereva wa bodaboda, Issa Kanjeche.

Alisema njia wanayotumia kukwepa abiria wa mbali na wasiowajua ni kuwaambia tu kwamba pikipiki haina bima.



Akieleza jinsi wezi wanavyowapora pikipiki, dereva mwingine wa bodaboda, Juma Hussein, alisema wezi hao hufika kituoni wakiwa kati ya wawili au watatu au hata mmoja na kila mmoja huomba apelekwe nje ya mji kupitia barabara moja.

Hata hivyo, alisema wakishafika nje kidogo ya mji, huomba `wachimbe dawa' kisha kuwakaba madereva wa bodaboda baada ya kuwatisha kwa bastola au visu kikubwa.

Hadi kufikia juzi, ni dereva mmoja tu (jina lake limehifadhiwa), ndiye aliyejeruhiwa katika paji la uso na waporaji hao, baada ya kujaribu kupambana na waporaji.

Taarifa za awali zinasema, wengi kati ya walioporwa pikipiki hizo, ni wale waliokopa kupitia taasisi za kifedha na ofisi zinazoaminika za kusaidia kuinua na kuimarisha uchumi wa wa jamii.

Polisi mjini hapa, wamethibitisha kuwepo kwa wimbi la uporaji wa pikipiki, ingawa haikuwa tayari kutoa ufafanuzi zaidi wa kama kuna baadhi ya wezi wameshakamatwa au pikipiki kupatikana.

# Watangazaji wa Ruangwa FM wapewa changamoto

**Na Abdul Mitumba, Ruangwa**

WAFANYAKAZI wa kituo cha Redio ya Jamii cha Ruangwa FM, wametakiwa kuwa wabunifu na kuandaa vipindi vyenye mvuto vinavyogusa jamii, ikiwemo kilimo.

Hatua hiyo itasaidia kituo kupata wasilikizaji wengi, ambapo baadhi yao wanaweza kutangaza biashara au kazi zao hatimaye kila upande kunufaika na uwezo wa redio hiyo kiuchumi .

Wito huo ulitolewa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi, Andrew Chikongwe, alipofanya mahojiano na gazeti la UELEKEO siku chache baada ya kutembelea kituo hicho na kuzungumza na wafanyakazi.

"Moja kati ya sifa za kukua kwa kituo cha redio, ni kuwa na wasikilizaji wengi.

Lakini wingi hauji kirahisi, ni lazima wafanyakazi wakiwemo watangazaji, wafanye kazi za ushawishi kwa weledi, bidii na maarifa," alisema.

Alisema ni muhimu waandaaji wa vipindi na watangazaji wakawa wabunifu, huku

Halmashauri ikiendelea kuboresha maslahi yao na kuhakikisha inawalipa kwa wakati licha ya kwamba pato kuu la halmashauri ni mazao ya kilimo, ikiwemo ufuta, korosho na mbaazi.

Kwa upade wao, wafanyakazi wa Ruangwa FM, waliahidi kufanya kila walilo nalo kuhakikisha jamii inapata matangazo yaliyo bora na kumhakikishia Mwenyekiti kwamba maelekezo yake wanayafanyia kazi.

"Tunafahamu jukumu letu kwa jamii. Kitu cha kipekee kwetu ni kuona redio sasa inasikika umbali mrefu hasa baada ya matengenezo makubwa ya studio na mifumo ya kurushia matangazo yaliyofanywa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UNISAF) ambayo imewekeza zaidi ya Sh. milioni 500 na kukifanya kituo kuwa cha kisasa," alisema Juma Mwelu maarufu 'Mzee wa Kuzungumziwa'.

Kwa sasa Ruangwa FM inasikika katika zaidi ya mikoa mitano nchini ikiwemo Lindi yenyewe, Mtwara, Ruvuma, Pwani na sehemu ya Mkoa wa Morogoro, tofauti na awali ambapo ilisikika wilaya tatu tu za Liwale, Nachingwea na Ruangwa za Mkoa wa Lindi.

**Tunafahamu jukumu letu kwa jamii. Kitu cha kipekee kwetu ni kuona redio sasa inasikika umbali mrefu hasa baada ya matengenezo makubwa ya studio na mifumo ya kurushia matangazo yaliyofanywa na Mfuko wa Mawasiliano.**



# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

## HII NI KERO

### Uchafu Soko la Ilala



SOKO Kuu la Ilala jijini Dar es Salaam, ni maarufu kwa uingizaji wa bidhaa mbalimbali za vyakula kutoka shamba na hatimaye kusambaza katika maeneo mbalimbali ya masoko au kumfikia mlaji wa mwisho.

Lakini Soko hili haliingiliki kipindiki cha mvua kutokana na tope jingi na maji machafu kutuama kutokana na miundombinu mibovu.

Wahusika mlione hili kwani kuna mlipuko wa magonjwa mengi kikiwemo kipindupindu.




## MAONI YA MHARIRI

# Rushwa ya ngono vyuoni, ipigwe vita kwa nguvu zote

JANA, Serikali ilikiri kuwepo kwa malalamiko ya rushwa ya ngono vyuoni.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, aliliambia Bunge jijini Dodoma kuwa kati ya mwaka 2020 na mwaka jana, zilipokelewa taarifa 11 za malalamiko ya vitendo vya rushwa ya ngono vyuoni.

Ridhiwani alisema kati ya malalamiko hayo, majalada tisa ya uchunguzi, yameanzishwa ambapo mawili yamefungwa baada ya kukosekana kwa ushahidi.

Ridhiwani aliyasema hayo alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalumu, Amina Daud Hassan, aliyetaka kufahamu kama serikali inatambua uwepo wa rushwa ya ngono kwa wanafunzi katika vyuo hapa nchini na hatua zilizochukuliwa.

Waziri Ridhiwani alisema jalada moja kati ya 11, limepata kibali cha kumfikisha mtuhumiwa mahakamani, majalada mawili yamependekezwa watuhumiwa wake wachukuliwe hatua za kinidhamu, jalada moja kesi imeshindwa mahakamani na majalada manne bado yanaendelea na uchunguzi.

Taarifa hii kwa hakika haipendezi na haijengi taswira nzuri kwa taifa letu. Rushwa ya ngono vyuoni, haina tofauti na wizi ama udanganyifu wa mitihani shuleni.

Mbaya zaidi wanaotuhumiwa kujihusisha na rushwa hiyo ya ngono vyuoni, ni watu wa kada iliyoelimika na inayofahamu kwa dhati kabisa athari za vitendo hivyo kwa taifa.

Ni dhahiri kwamba rushwa ya ngono vyuoni, hufanywa kwa lengo la kuwasaidia wanafunzi wafaulu mitihani yao.

Lengo halisi la mtihani, ni kumpima mwanafunzi kuona kama ameelewa kile alichofundishwa darasani kwa nadharia ama kwa vitendo.

Athari za mwanafunzi aliyefanya udanganyifu wa mitihani, hautofautiani na yule aliyesaidiwa mitihani kupitia rushwa ya ngono.

Tunapaswa kujiuliza, je; tunataka kuandaa taifa la namna gani? Taifa lolote lile lazima liwe na wanasayansi, wahandisi, madaktari, walimu na watu wa kada mbalimbali za kitaaluma ambazo walizipata kupitia vyuo walivyosoma.

Sasa inapotokea rushwa ya ngono ama udanganyifu wa mitihani, tutarajie kuwapata madaktari, wanasayansi, wahandisi, marubani wa aina gani?

Kwa maana ipo hatari mno ya kuwapata madaktari ama wataalamu hao kwa ujumla, waliofaulu kwa `kuiba' mitihani na si kwa uwezo wao.

Ni jambo la hatari mno na hatuna budi lipigwe vita kwa nguvu zote na kwa hili iwe kwa mtoa rushwa na mpokeaji wa rushwa ya ngono ili iwe mfano kwa wengine wanaofikiria kufanya kitendo hicho cha aibu.

## Wasiliana nasi

**Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000
**Mhariri wa Habari:** +255768411003
**Mhariri Michezo:** +255787559090
**Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825
**S. L. P:** 15110, Dar es Salaam
**Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro
**Jengo la:** Aura Mall
**Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532
**Email:** uelekeohabari@gmail.com

## JICHO LANGU

Na Abdul Mitumba, Ruangwa

# Rushwa ya ngono: Takukuru, Polisi, Mahakama kaeni macho

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (Takukuru), ni taasisi ya umma iliyopewa dhamana ya kusimamia na kufuatilia utendaji kazi wa mifumo mbalimbali ikiwa ni pamoja na mfumo wa uchaguzi kwa ajili ya kubaini mianya ya rushwa.

Taarifa za wasimamizi na wachunguzi wa chaguzi za Serikali za Mitaa na zile za Wabunge na Urais zilizopita, imebaini kuwepo kwa viashiria vya rushwa hasa ya ngono katika chaguzi zote.

Hata hivyo, eneo hili huwa haliko wazi kwani waathirika husita kutoa taarifa, hasa pale ambapo walilazimika kutoa rushwa ili wateuliwe, au wapewe wadhifa fulani kwenye mchakato wa uchaguzi.

Hivyo basi, kwa kutambua ukubwa wa tatizo hili, Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) ukishirikiana na Wanawake Wanamtandao wa Katiba, Uchaguzi na Uongozi na mitandao mingine ya Tapo la ukombozi wa wanawake, wataitaka Takukuru kufanya mambo yafuatayo kuelekea chaguzi zijazo.

> **Aina hii ya rushwa siyo tu kwamba inadhalilisha utu, bali inakiuka haki za msingi za mwathirika hasa pale anapolazimika kubadilisha ngono ili kupata haki zake, kama vile uteuzi wa kugombea nafasi za uongozi ndani ya chama.**

Mosi, ianze sasa kujikita katika kuelimisha raia kuhusu suala la rushwa, hususan, rushwa ya ngono na madhara yake katika jamii.

Katika eneo hili, Takukuru inawajibu wa kushirikiana na asasi za kiraia katika kuelimisha umma kuhusu athari na madhara ya rushwa ya ngono ikiwemo kudhalilisha utu wa mwathirika.

Aina hii ya rushwa siyo tu kwamba inadhalilisha utu, bali inakiuka haki za msingi za mwathirika hasa pale anapolazimika kubadilisha ngono ili kupata haki zake, kama vile uteuzi wa kugombea nafasi za uongozi ndani ya chama.

Mbili, Takukuru ihakikishe inashirikiana na asasi za kiraia katika kuwajengea uwezo wanawake wanaowania nafasi mbalimbali kwenye uchaguzi ili wawe na uthubutu wa kuwataja wote wanaowashawishi kubadilisha haki zao kwa ngono ili kuvunja ukimya uliopo kwenye changamoto hii.

Tatu, Takukuru ihakikishe vitendo vyote vya rushwa pamoja na rushwa ya ngono vinachukuliwa hatua stahiki ikiwa ni pamoja na hatua za ki mahakama kama zilivyoainishwa kwenye sheria husika.

Tatu, vyombo vyote vinavyosimamia haki na utawala wa sheria kwenye uchaguzi ambavyo ni Jeshi la Polisi na Tume ya Haki za Binadamu zinasimama imara.

Hapa Takukuru itawajibika kushughulikia kesi zote zitokanazo na uchaguzi ambazo kwa kawaida zinahitaji gharama kubwa, ni muhimu zikawekewa utaratibu maalumu katika kusikilizwa kwake ili kuwapa nafuu walalamikaji hasa wanawake.

Nne, mbali na vyombo hivyo vya kusimamia haki, TGNP na washirika wake wanaamini pia kwamba, mahakama nayo ina nafasi kubwa ya kuhakikisha chaguzi zote zinakuwa za haki kisheria.

Ni muhimu ikaeleweka kuwa, wanawake wengi wagombea na hata wapigakura watakuwa na uhitaji wa msaada wa kisheria wakati wote ili waweze kutoka malalamiko yao bila woga.

Tano, kesi zinazohusu rushwa ya ngono zinahitaji ufaragha mkubwa ili wahanga wawe huru kujieleza na kujitetea. Mahakama ihakikishe kunakuwa na ulinzi kwa wanawake wakati wa kutoa malalamiko yao mahakamani.

Sita, katika kutenda haki, Jeshi la Polisi nalo lina nafasi kubwa katika kuwawezesha wanawake kupata haki zao pale zinapokiukwa.

TGNP na washirika wake wanalitaka jeshi hilo kuharakisha kupokea na kupeleka mahakamani malalamiko ya wanawake, wawe wapiga kura au wanaowania kuteuliwa ndani ya vyama vyao.

Saba, Tume ya Haki za Binadamu zisimamie utekelezaji wa maadili na ukiukwaji wa haki za wanawake katika kila chakuzi.

Wanamtandao wa Wanawake, Katiba na Uchaguzi, na mitandao mingine ya Tapo la ukombozi wa wanawake kwa sauti moja wanasema kwamba, ucheleweshwaji wa haki ni sawa na unyimaji wa haki.

# KATIBU WA NEC ITIKADI, UENEZI NA MAFUNZO YA CCM, PAUL MAKONDA AKIPEWA UCHIFU NA WAZEE WA SIMIYU KATIKA MUENDELEZO WA ZIARA ZAKE MIKOANI














# Mambo 5 ya kujua kuhusu nimonia



**Mwandishi wa BBC**

NIMONIA (Pneumonia) ni maambukizi kwenye mapafu maarufu kama homa ya mapafu na mara nyingi husababishwa na bakteria au virusi; ni ugonjwa unaoathiri mfumo wa kupumua ikiwamo kwa watoto lakini pia watu wazima wanaweza kuugua ugonjwa huo.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), watoto 740,000 walio chini ya umri wa miaka mitano walifariki kutokana na homa hiyo ya mapafu kwa mwaka 2019.

Kila Novemba 12 ya mwaka ulimwengu huadhimisha, "Siku ya Kimataifa ya Kupambana na Pneumonia."

## Pneumonia au homa ya mapafu ni nini?

Kwa lugha nyepesi ni maambukizi yanayotokea katika mfumo wa kupumua na mara nyingi maambukizi haya hutokana na virusi, bakteria au hata kuvu.

Maambukizi yakitokana na bakteria, maji na usaha hukusanyika katika eneo linalofanya kazi kuchuja hewa ya oksijeni na carbon dioxide wakati wa upumuaji.

Hatua hiyo inafanya mfumo wa upumuaji hewa kuwa vigumu, hatua inayosababisha pia kiwango cha oksijeni kupungua katika damu mwilini, maambukizi yanaweza kuwa mepesi au mara nyingine yanasababisha hata kifo cha mwathiriwa.

## Dalili za homa ya mapafu ni zipi?

Mtu ye yote anaweza kuugua homa ya mapafu na dalili zake ni pamoja na kupata matatizo ya kupumua kuongozeka kwa mapigo ya moyo, joto mwilini, kutetemeka, kutokwa na jasho mwilini, kukohoa, maumivu kifuani, kuumwa na kichwa, kichefuchefu, kutapika na kuharisha.

Wataalam wanasema ni muhimu kutambua aina ya homa ya mapafu kwa kufanyiwa utafiti wa maabara na kupata matibabu.

WHO linasema kwamba iwapo maambukizi yametokana na bakteria au virusi madhara yake hayana tofauti, yako sawa.

Hata hivyo dalili hutofautiana kidogo iwapo homa hiyo inatokana na maambukizi ya virusi, basi baadhi ya dalili anazokuwa nazo mgonjwa ni pamoja na kikohozi, joto mwilini, mafua na kupata matatizo ya kupumua.

## Vipi unaweza kutambua mtoto anaugua homa ya mapafu?

**Joto mwilini**

Watoto wanaweza kupata joto mwilini kwa sababu tofauti, mara nyingi joto mwilini hutokea wakati mwili unapambana na ugonjwa.

Lakini iwapo joto ni kali au halishuki hata unapompatia mtoto dawa ni lazima umfikishe mtoto kituo cha afya na kumuona daktari.

## Matatizo ya kupumua

Upumuaji wa watoto huwa tofauti kila saa mchana. Wao hupata matatizo ya kupumua wanapopata maambukizi ya homa ya mapafu.

Baadhi hutoa sauti kama filimbi kuashiria ugumu wanaopata kupumua. Hapa mzazi unahitaji kuwa na uangalifu mkubwa.

## Uchofu

Mapafu hujaa maji kutokana na homa hii, hali hiyo inasababisha shida ya kupumua, mtoto anahisi kuchoka, iwapo mtoto wako anaonekana kuchoka saa zote, basi ni muhimu apate ushauri wa daktari haraka iwezekanavyo.

## Je homa ya mapafu inatibiwa vipi?

Ni muhimu kuzitambua dalili na mapema, na ni rahisi kutambua homa ya mapafu kwa watoto walio chini ya miaka mitano.

Aidha anapopata matatizo ya kupumua ni muhimu kumfikisha hospitalini haraka iwezekanavyo, virusi ndani ya mapafu vinaweza kuchukua siku kadhaa hadi wiki kusambaa mwilini, maambukizi ya bakteria yanaweza kutibiwa kwa dawa za antibiotics.

Hata hivyo, iwapo maambukizi ni makali huenda mgonjwa akahitaji kulazwa hospitalini, wataalamu wanashauri kwamba wagonjwa wanaweza kupoa haraka kwa kuchukua hatua kama vile kupumzika na kunywa maji mengi.

Jarida hili haliuzwi

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

Uelekeo

JARIDA

# Jungu Kuu

| Jumatano Januari 31 - Februari 6, 2024 |






# Makonda anavyosaidia kutekeleza Ilani ya CCM

UK. 12 & 13

Siasa

Na Mwandishi Wetu

# Waliosemwa wamechoka 2013, bado wapo Chadema -2




WIKI iliyopita tulianza kujikumbusha waraka wa Mkakati wa Mabadiliko uliosambaa mitandaoni mwaka 2013 na kusababisha baadhi ya viongozi waandamizi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) waliotuhumiwa kuandaa mkakati huo kuondolewa.

Baadhi ya waliofukuzwa ni aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu wa Chadema, Zitto Kabwe (sasa kiongozi wa ACT-Wazelendo), aliyekuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chadema Profesa Kitila Mkumbo (sasa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji) na aliyekuwa Mwenyekiti wa Chadema Mkoa wa Arusha, Samsoni Mwigamba

Ulikuwa ni mkakati ulioonesha kuchoka na kukosa mbinu kwa uongozi uliokuwa madarakani wakati huo na hivyo kutaka kuwepo kwa mabadiliko ili kukihuisha chama hucho.

Katika sehemu ya kwanza tulioangalia wiki iliyopita, mkakati ulionesha kwamba viongozi wa sasa walioingia madarakani 2004, wamekuwa wazito kung'atuka madarakani na kupisha damu mpya kuongoza chama hicho.

Pia walidaiwa kutumia mbinu za maandamano na harakati nyingine kama Movement For Change (M4C) ambazo hata hivyo kwa majibu wa waliokuwa wakitaka mabadiliko, hazikuzaa matunda ya maana.

Tukaona kwamba licha ya mbinu hizo, Chadema hakikufanya vizuri katika chaguzi kubwa na ndogo katika kipindi cha uongozi wa viongozi hao hadi wakati waraka wa mabadiliko unaandikwa.

Leo tunaendelea na sehemu ya pili ya waraka huo wa kutaka mabadiliko ndani ya Chadema uliovuja na kusababisha akina Zitto Kabwe kutimuliwa. Pengine kuna mabadiliko ya utendaji lakini viongozi waliodaiwa takribani miaka 11 iliyopita kwamba wamechoka na hawawezi kuifikisha mbali Chadema bado wapo madarakani.

## UBADHIRIFU

Matumizi ya fedha za taasisi. Hakuna mtu anayejua hivi sasa fedha za chama zinatumikaje zaidi ya kakikundi ka watu watatu, yaani mkuu kabisa, mtendaji mkuu na mkuu wa fedha kwenye taasisi yetu.

Maamuzi ya vikao hayaheshimiki tena na mabwana hawa. Baada ya uchaguzi wa 2010 vikao halali vilielekeza kiasi na aina ya fedha ambazo hazitaguswa bali zitunzwe kwenye akaunti maalumu kwa ajili ya uchaguzi wa 2015. Lakini leo (2013) si tu akaunti hiyo haina fedha bali hakuna akaunti yoyote yenye fedha. Watu watatu ndo wanaamua fedha zitumikeje.

Mfano mwingine ni maamuzi ya kikao cha juu mno cha hivi karibuni kilichoamua kwamba kiasi cha fedha inayotoka serikalini kipelekwe kwenye mikoa na wilaya na kiasi kingine kipelekwe kwenye kanda. Leo ni mwezi wa tano maamuzi hayo hayajatekelezwa. Lakini kuna michango ya watu binafsi kama yule mtanzania mwenye asili ya kihindi, hizo nazo hazijulikani zimechukuliwa lini kwa mfumo gani, zikatunzwa wapi na hatimaye zimetumikaje.

Hapo hatujataja fedha zinazopatikana kutoka kwenye fundraising events mbalimbali kama ile ya Dar es salaam na Mwanza. Hizo nazo hazijawahi kuonekana na walioendesha hizo fundraising, uaminifu wao kwenye masuala ya fedha ni questionable.

Taarifa za fedha. Tokea baada ya uchaguzi wa 2010 mpaka leo (2013), hakuna kikao chochote kilichowahi kupokea na kujadili hadi mwisho ripoti ya mapato na matumizi ya fedha za taasisi. Kila kikao agenda hiyo inarushwa kiaina. Wanaojua mchezo huo ni watu watatu tu tuliowataja hapo juu na malengo ya kurusha hiyo agenda kila wakati na kukwepesha isijadiliwe pia wanayajua wao.

Ni dhahiri tukiendelea na hawa watu tutafika 2015 tukiwa hatuna pesa hata ya kuweka mawakala kwenye vituo na tutapigwa tukiwa tumesimama. Kwa kiasi kikubwa mkuu aliyepo anatengeneza mazingira yaleyale ya mwaka 2005 na 2010 ya kutaka chama kiwe hakina hela ili ikifika wakati wa uchaguzi kimpigie magoti. Kisha atatoa pesa bila kumbukumbu zozote na mara baada ya uchaguzi anapeleka lundo la deni na kudai alipwe hela aliyekikopesha chama wakati wa uchaguzi. Alifanya hivyo katika chaguzi za 2005 na 2010.

Wakati wote wa kampeni za mwaka 2010, kwa mfano, taasisi yetu ilihangaika sana kwa kukosa hata hela ya kununua maji kwa wajumbe wa ngome. Lakini ajabu ni kwamba baada ya uchaguzi mkuu wa taasisi na baadhi ya wapambe wake walilete deni kubwa la takribani shilingi milioni mia tano akidai kuwa walikikopesha chama. Taasisi imewalipa pesa zote hizi kwa muda mwaka mmoja. Sasa anatengeneza mazingira hayohayo kwa ajili ya uchaguzi wa mwaka 2015.

## MAPATO YA ZIADA

Hakuna mipango ya kukipatia chama mapato ya ziada kutoka nje ya chama. Kimsingi wakuu waliopo hawana hata ndoto ya namna ya kupata fedha za ziada.

Wanachokijua ni kukusanya 'sadaka' kwenye mikutano ya hadhara na kuwapatia kazi watu wanaoonekana kuwa matapeli eti waendeshe harambee za kuchangisha fedha kwa njia ya matukio.

Mawazo mazuri kama lile la kuanzisha kampuni la uwekezaji la taasisi yetu litakalowekeza kwenye miradi mbalimbali, halijawahi kufanyiwa kazi, na hivyo uanzishaji wa miradi mbalimbali ya kuiingizia taasisi fedha imebaki ndoto ya mchana.

Hatuwezi kufika hata siku moja bila fedha. Hata uchaguzi wa wenzetu wa hapa jirani juzi juzi wakuu wetu ingawa walishiriki lakini hawaonekani kama wamejifunza chochote.

## KUBAKI MADARAKANI

Ili kuhakikisha wakuu wanabaki madarakani, wameanzisha vikundi vikundi ndani ya taasisi yetu. Siku hizi ni rahisi sana kuambiwa kwenye taasisi yetu eti huyu ni wa boss na huyu ni wa dogo. Na wale walio wa boss kwa kuwa boss ndo anashikilia raslimali za taasisi anatumia mfumo haramu kuwaneemesha watu wake kwa kutumia raslimali za taasisi na kuwakandamiza wote wanaoonekana wanapishana naye kimtazamo.

Jambo hili limewaibua wachumia tumbo, wapenda madaraka, na vibaraka lukuki wanaokwenda kujipendekeza kwa wakuu wa taasisi kwa malengo ya kujinufaisha binafsi.

Katika kufanya hivyo vibaraka hao wamekuwa wakiwaendea wakuu wa taasisi na kuwajaza maneno mabaya dhidi ya viongozi wenzao na kuzidi kuwafarakanisha viongozi wa juu.

Kuna mchezo umeanzishwa na wakuu wa taasisi unaitwa ulinzi wa chama uliogawanyika katika makundi mawili yaani visible na invisible. Visible ni ule unaoonekana ambao uko chini ya kikosi chetu chekundu ambacho kinajulikana kwa kila mtu lakini invisible wanajulikana kwa mkuu wa taasisi na mtendaji mkuu peke yake.

Wanafanya kazi kwa maelekezo ya wakubwa hao wawili na hawajulikani kwa viongozi wengine wa juu. Ni hawa hawa ambao wanatumika vibaya pale wanapoleta taarifa za kiintelijensia ambazo zinawahusisha viongozi wasiopendwa na wakuu na usaliti dhidi ya taasisi.

Hakuna kamati maalumu inayowathibitisha maaintelijensia hao bali wakuu wenyewe wanawachukua wanaowataka. Ni katika mfumo huu wa kipuuzi mida eight amekuwa akitumika vibaya kwa kumshambulia mtendaji mkuu msaidizi hadharani kwa kutumia mitandao ya kijamii na wakuu wanafurahia na kumlipa pesa.

## UDHAIFU WA BOSI

Mtendaji mkuu ni dhaifu mno na ni mara nyingi sana tumeshuhudia mkuu wa taasisi akifanya mambo ya kiutendaji kinyume na utaratibu kama vile yeye mwenyewe kuja kwenye kamati ya makatibu na wakurugenzi na kupangua mipango yao na ku-inject ya kwake na mtendaji mkuu kuadopt tu kana kwamba yeye hawezi kupanga mambo ya kiutendaji.

Hata tunapokuwa kwenye operesheni maalumu tumeshuhudia mkuu wa taasisi ndo akipanga watendaji, posho zao na hata kusimamia matumizi ya pesa na shughuli mbalimbali za kiutendaji.

Udhaifu wa mtendaji mkuu ni udhaifu wa mkuu wa taasisi kwa kuwa amemteua yeye mara mbili tena mara ya pili alileta jina moja mbele ya Baraza la juu kuonesha kwamba aliridhika na utendaji wake kiasi cha kutotaka kumpambanisha na mwingine.

Lakini baada ya kumpendekeza mara ya pili ndipo tumeshuhudia yeye kuingilia kati mara nyingi sana mambo ya kiutendaji kana kwamba anamfichia aibu mtendaji wake. Swali kwa nini alimteua tena? Jibu lake litakuwa rahisi tu kwamba ni kwa sababu mtendaji huyu ni passive kwake (ndiyo mzee) kwa kila takwa la mkuu wake.

*Itaendelea*



Hamisi Kibari

TUKUBALIANE KUTOKUBALIANA

Simu: 0758143457

# Waendeshaji Afcon wasaidiwe kujitambua

KIKAO cha 35 cha Wakuu wa Nchi na wa Serikali wa Umoja wa Afrika (AU), kilichoketi Februari 5, mwaka 2022, pale Addis Ababa, Ethiopia, kilipitisha Kiswahili kuwa lugha ya kazi ya AU. Pia kilipitisha lugha hiyo kuwa ya mawasiliano, siyo tu kwa umoja huo, bali kote Afrika.

Kabla ya hatua hiyo, Umoja wa Afrika ulikuwa na lugha tano za kazi na zote hazina asili ya Afrika. Lugha hizo ni Kiingereza, Kifaransa, Kireno, Kiarabu na Kihispania. Hatua hiyo iliyochelewa sana kuja, inafanya Kiswahili kuwa lugha ya sita ya kazi ya Umoja wa Afrika.

Kikao hicho kiliiagiza Tume ya AU kuchukua hatua zote muhimu ili kutekeleza uamuzi huo ifikapo Julai 2023. Yaliyojitokeza kwenye michuano ya mataifa ya mpira wa miguu Afrika (AFCON) inayoendela pale nchini Ivory Coast, mintarafu matumizi ya lugha ya Kiswahili, yanatia shaka kama hilo limefanyika.



Patrice Motsepe

**KUZUNGUMZWA NA MAMILIONI**

Ifahamike kwamba Kiswahili ndio lugha ya Kiafrika inayozungumzwa na watu wengi kuliko lugha nyingine yoyote na inatajwa kuwa lugha ya 10 kwa wingi wa wazungumzaji duniani kote.

Wakati Kiswahili kinakadiriwa kuwa na wazungumzaji zaidi ya milioni 200, lugha ya nyingine ya Kiafrika inayofuatia ni Kiyoruba kinachokadiriwa kuwa na wazungumzaji milioni 50. Kwa hiyo Kiswahili kinakizidi Kiyoruba mara tatu zaidi kwa idadi ya wazungumzaji.

Hatua hiyo ya AU ilielezwa na wadau kwamba ni msukumo mpya katika kukifanya Kiswahili kuwa 'lingua franka' barani Afrika, na kwamba ni hatua muhimu yenye kulinufaisha bara la Afrika na ulimwengu kwa ujumla kwa kuwa na lugha ya mawasiliano ya kimataifa yenye asili ya bara hili.

**WADAU WAPENDEKEZA**

Wadau walihimiza kila mwafrika kufanyia kazi hatua iliyofikiwa na AU ili kuanza kupunguza utegemezi wa Afrika kwa lugha za kigeni katika mawasiliano rasmi. Wakashauri uwe mwanzo wa kuenea kwa Kiswahili na kukuza Uanamajumui wa Afrika (Pan-Africanism).

Hivyo, ilitazamiwa kwenye mikusanyiko mkubwa kama wa michuano ya Afcon, Kiswahili pia kingepigiwa chapuo lakini mambo yamekuwa kinyume.

**HOFU YA WADAU**

Hata hivyo, wapo wachambuzi wa mambo walisema kwamba kampeni ya kusambaza Kiswahili, inaweza kukabiliwa na changamoto kadha wa kadha.

Kwa mfano, Profesa Obuchi Moseti, mhadhiri wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Moi cha nchini Kenya, alisema kuwa lugha hizi za kigeni zimeimarika na kuwekwa kimkakati kwa ajili ya mawasiliano, diplomasia na biashara ya kimataifa na kwamba pengine haitakuwa rahisi sana kuzibadilisha na lugha ya kiafrika.

Lakini akasema ili Kiswahili kiweze kufanikiwa kupenya zaidi Afrika kutategemea sana utashi wa kisiasa.

Profesa mwingine kutoka Kenya, Chege Githora, aliwaambia wanahabari kwamba tatizo lingine kubwa la Waafrika ni kusumbuliwa na kasumba pamoja na ushamba wa kuthamini vitu vya wakoloni kuliko vya kwao ikiwemo lugha!

"Huwezi kuamini, bado kuna wajinga wanaona lugha kama Kifaransa, Kiingereza na Kireno kwamba ni lugha zenye nguvu," alisema.

**MBUMBUMBU WA AFCON**

Kilichokuwa kinazungumzwa na maprofesa hao wa Kenya kilijitokeza kwenye michuano ya mpira wa miguu ya Afrika (Afcon).

Ilikuwa ni kwenye mkutano wa wanahabari kabla ya mechi ya timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars) na timu ya Taifa ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) wakati mabosi wa Shirikisho la Mpira Afrika (CAF) walipowazuia na kuwapa onyo kali Nahodha wa Stars, Mbwana Samatta na kocha wake, Hemed Morocco wasitumie lugha ya kiswahili kuzungumza!

Mabosi hao wa CAF walidai eti Kiswahili hakitambuliki na kwamba lugha za kutumia ni Kingereza, Kifaransa, Kireno na Kiarabu!

Nimekuwa ninajiuliza, kweli Tume ya AU imefanya kazi yake kadri ya maagizo iliyopewa na wakuu wa nchi na serikali wa bara hili?

Inashangaza kuona hao jamaa wakipinga lugha ambayo tayari imepitishwa na kubarikiwa na Umoja wa Afrika (AU). Hili kwa kweli halikubaliki na ni jambo linakotakiwa kupingwa kwa kila namna. Pengine ni vyema hata AU ikajitokeza kukemea kilichotokea.

Ajabu ni kwamba, Rais wa CAF, Patrice Motsepe, bilionea anayetokea Afrika Kusini, nchi yake tangu mwaka 2018 iliidhinisha Kiswahili kuwa lugha ambayo inafundishwa katika shule za umma na za binafsi kote nchini humo.

Shule husika ni zile ambazo hadi 2018 zilikuwa tayari zinafundisha lugha nyingine za kigeni kama vile Kifaransa, Mandarin na Kijerumani.

Hatua hii ya Afrika Kusini ilikifanya Kiswahili kuwa lugha ya kwanza ya Kiafrika kufundishwa shuleni nchini humo. Sijui Motsepe hana habari?

**JUHUDI ZAIDI ZATAKIWA**

'Umbumbumbu' uliofanywa na CAF unatufundisha kwamba juhudi zaidi zinatakiwa kufanywa katika kueneza Kiswahili Afrika.

Baada ya mkutano ule wa AU uliopitisha matumizi ya Kiswahili, katika moja ya maandiko kwenye vyombo vya habari ilipendekezwa kwamba ni vyema AU iunde kamati au chombo maalumu chenye mamlaka ya kuelimisha nchi zote kuhusu umuhimu wa kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya Afrika.

Kwamba jukumu kubwa la kamati hiyo liwe ni kushawishi nchi za Kiafrika kuunga mkono wazo hilo kwa kuwafikia wadau wa ndani na nje ya Afrika, ili viongozi wa kisiasa wawe na utashi na hata kuwa tayari kufadhili programu za kuimarisha na kusambaza Kiswahili.

Kwamba kamati hiyo pia iwe na dhima ya kufanya utafiti na kubuni mikakati ya kukuza Kiswahili barani Afrika na hasa namna ya kupata rasilimali muhimu za kusaidia kueneza Kiswahili. Ikashauriwa kuanza na mafunzo kwa walimu wa Kiswahili na mbinu za kujifunza lugha hiyo kama lugha ya pili kwa nchi ambazo kwa sasa hazizungumzi Kiswahili.

Kupitia ufadhili, inashauriwa maktaba mbalimbali Afrika ziwe na vitabu vya Kiswahili huku mikusanyiko mikubwa ikiwemo michuano kama ya Afcon ikitumika katika kuhamasisha Kiswahili kote barani Afrika.

Pamoja na kampeni nyingine za kuhamasisha lugha hii adhimu, inashauriwa pia kuwe na makongamano barani kote yakielezea umuhimu wa kuwa na lugha ya Kiafrika sambamba na vitabu na wanafunzi waliojifunza Kiswahili na kufikia viwango fulani vya ustadi wa lugha.

Mashindano ya uandishi wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili kwa nchi ambazo hazizungumzi Kiswahili yakiambatana na zawadi za kuvutia yanaweza pia kusaidia kuhamasisha kuenea kwa Kiswahili.

Inashauriwa pia kwamba sera za lugha katika bara zima la Afrika hazina budi kubadilika kwa kujielekeza kukifanya Kiswahili kuwa somo la lazima shuleni au kama lugha ya kujifunzia katika elimu rasmi.

Wadau wanasema kanuni nyingine za AU na Umoja wa Mataifa zinaweza kuimarisha juhudi za kukuza Kiswahili kwa ujumla. Kwa mfano, watu wanaoingia Afrika kwa ajili ya uwekezaji wa muda mrefu au kwa madhumuni ya elimu wanaweza kuhitajika kusoma na kupata umahiri wa Kiswahili ndani ya muda uliowekwa.

Pia inaweza kuamriwa kwamba mtu yeyote anayehutubia mikutano ya AU awe na ujuzi wa kutosha wa Kiswahili, hata kama si kwa ustadi wa asilimia 100.

Watanzania tunatakiwa kuwa msitari wa mbele kupigia debe hatua iliyofikiwa na AU na kuhakikisha mambo hayarudi nyuma. Pengine ni wakati mwafaka kwa viongozi wetu kupenda kuhutubia kwa Kiswahili kwenye mikutano ya kimataifa au inayowahusisha watu kutoka ughaibuni na kuwapa kazi wakalimani kutafsiri hata kama wanajua Kiingereza au Kifaransa.

Kiswahili kama bidhaa, kusambaa kwake kunaweza kuwa na manufaa ya ziada kwa Watanzania na miongoni mwa wanufaika ni walimu wa Kiswahili, waandishi wa vitabu na watengeneza filamu kwa lugha adhimu ya Kiswahili na kadhalika na kadhalika.

Hata kule Ivory Coast akina Samatta walitakiwa kugoma kuzungumza Kiingereza. Huwezi, kwa mfano, kumuamrisha Mchina azungumze lugha nyingine hata kama anaijua. Tufike hapo.

Siasa

# Makonda anavyosaidia kutekeleza Ilani ya CCM

- **Hii ni njia nzuri kumsaidia Rais Samia kumaliza kero za wananchi**



**Na Hamid Yassin**

KATIBU wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda yupo kwenye ziara ya awamu ya kwanza ya mikoa kumi ambako pamoja na kuangalia mambo mengi lakini rasmi ni kukagua utekelezaji wa Ilani ya chama hicho kilichopewa ridhaa na wananchi kuongoza nchi yetu.

Katika ziara hizo Makonda mbali ya kufanya vikao vya ndani na viongozi wa CCM na serikali, pia anafanya mikutano ya hadhara na wananchi.

Katika mikutano hiyo mbali ya kusikiliza kero zao binafsi, pia anaangalia kama yale yaliyoahidiwa na CCM kwenye kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 kupitia Ilani yao ya uchaguzi yanatekelezwa na kusimamiwa vizuri na watendaji waliopewa dhamana ya kufanya hivyo.

Hii kazi aliyojitwika Makonda si ya mchezo, ni jukumu pevu kwani moja kwa moja anagusa masilahi ya watu, hivyo mbali ya kusifiwa na wananchi wengi lakini anajijengea chuki na uadui kwa baadhi ya viongozi wenzake ambao wanaona anawachimbachimba; watoto wa mjini wanasema anataka kuwatilia 'vitumbua' vyao mchanga!

Hata hivyo, Makonda ameweka wazi kwamba yote anayoyafanya yanatokana na uwezo wa Mungu sambamba na heshima aliyopewa na Mwenyekiti wa chama hicho, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

"Ubingwa wangu unatokana na uwezo wa Mungu na nafasi aliyonipa Mwenyekiti na Rais wetu, Dk. Samia. Yeye ndiye kafanya leo hii mnione hapa, mkifurahia haya ninayofanya mjue kabisa ninafanya kwa niaba yake Mwenyekiti wetu, hivyo sifa, shukrani na pongezi zinastahili kwake na si mimi," Makonda aliyesema hayo alipozimamisha msafara wake na kuzungumza na wazee, wanawake na vijana wajasiriamali katika Kata ya Pongwe akitokea Wilaya ya Tanga.

Kila anapopita lazima awasimamishe au kuwapigia simu viongozi kujibu zile kero anazozipata toka kwa wakazi wa maeneo hayo husika.

Ameshawaunganisha wananchi na mawaziri, wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya, wabunge, wakurugenzi wa halmashauri, manispaa na hata wale wa mikoa kujibu kero mbalimbali zinazowakabili.

Si hao tu watendaji wa Serikali wanaokumbana na patashika za Makonda, bali hata wale wa ndani wa chama chake nao hayuko nyuma katika kuwakumbusha wajibu na majukumu yao, kama alivyotoa maelekezo ya CCM inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ya kuwataka wenyeviti wa chama hicho wa wilaya zote nchini kutoa ripoti za Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wazembe kwenye maeneo yao.

**WAZEMBE, WABADHIRIFU HAWAKOSEKANI**

Makonda anasema CCM inaelewa kuwa, kuna Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wazembe kwenye maeneo yao ya kazi wanaosababisha kukwama kwa maendeleo au kuwa chanzo cha migogoro miongoni mwa wananchi na wakati mwingine hata na serikali.

Mkuu huyo wa zamani wa Wilaya ya Kinondoni na Mkoa wa Dar es Salaam anasema kuwa, aina ya viongozi kama hao wasiowajibika ndio wale ambao wakiona viongozi wa kitaifa wanakwenda kwenye maeneo yao huwakamata wananchi wenye nia ya kusema kero na changamoto zao na kuwaweka ndani ili wasipate fursa ya kuongea wala kuonesha mabango yao.

Mwenezi huyo ametamka kamwe CCM haitawaonea haya viongozi wa aina hiyo bali itaendelea kuwashughulikia ili kuendelea kulinda imani iliyojijengea kwa miaka mingi mbele ya wananchi.

**KUMALIZA KERO YA UMEME**

Januari 21 akiwa wilayani Muheza mkoani Tanga, Makonda alikumbusha kwamba zaidi ya shilingi bilioni sita zinatumika katika mradi wa umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere na kufikia mwezi Machi mitambo tisa itakuwa imewashwa tayari kuunganishwa kwenye gridi ya taifa ambapo taifa linakwenda kupata ongezeko la zaidi ya megawati 2000 za umeme.

Katika kuelezea dhamira hiyo ya CCM kuhakikisha kero ya kukatika kwa umeme mara kwa mara inabaki historia nchini , Makonda anabainisha kwamba, kupitia kikao cha Halmashauri Kuu ya CCM Taifa walimwita Naibu Waziri Mkuu Kassim Majaliwa na Waziri wa Nishati, Doto Biteko ambaye aliwaambia mikakati yote ya serikali inavyokwenda katika kumaliza tatizo la kukatika kwa umeme na ukamilishwaji wa miradi mikubwa ya umeme.

Anasema pia walielezwa ahuweni ya gharama za upatikanaji sambamba na wananchi wote kuunganishiwa umeme hadi vijijini.

Mwenezi Makonda aliwaambia Wana-Muheza kwamba, dhamira ya Mwenyekiti wa CCM na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia ni kuhakikisha kero hii na kilio kikubwa cha umeme nchini inaondoka kwani wananchi wengi wanategemea umeme kwenye shughuli zao nyingi wanazofanya.

**KUSUASUA KWA MIRADI**

Katika ziara yake hiyo ndefu iliyoanzia Unguja Zanzibar na kupita kwenye wilaya na



mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Kilimanjaro, Singida, Tabora na Shinyanga; mpaka sasa Makonda amekutana na kadhia ya kusuasua kwa miradi kadhaa ya serikali.

Baadhi ya miradi hiyo ni ya maji, ujenzi wa zahanati, hospitali, shule za msingi na sekondari huku wasimamizi wake wakishindwa kutoa maelezo ya kuridhisha wakati mafungu ya fedha walishapata.

**TUMPE MAUA YAKE**

Naam; huyo ndiyo Paul Makonda ambaye hakuna dhambi nikisema ni kiongozi wa mfano kwa wengine kwa jinsi anavyofanya kazi ya kuwaokoa wananchi na adha mbalimbali kote anapopita kwenye hii ziara yake ndefu ya kuzunguka nchi nzima.

Makonda ni mpambanaji anayekerwa sana kuona kero za wananchi wa kawaiuida mitaani haziondoki.

Makonda hakuanza haya leo baada ya kutoka 'likizo' ndefu ya takribani miaka mitatu, tuliona kazi nzuri aliyoifanya tangu wakati wa mchakato wa Katiba pendekezwa, alipokuwa Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni na hadi pale alipokabidhiwa wadhifa wa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam wakati wa Serikali ya Awamu ya Tano.

Alipokuwa kiongozi mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam hakuna ambaye hakuona juhudi zake za kurekebisha madudu yaliyopandikizwa na watu waovu na hasa wapiga dili kama ufisadi maofisini, dhuluma ya kila aina kwa wananchi na hasa walioporwa viwanja, nyumba na mali zao.

Tuliona jinsi Makonda alivyowaumbua watu hao na wengine kuwatia ndani kutokana na madaraka aliyokuwa nayo kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu.

Tulishuhudia Makonda akifanya kazi za kishujaa kama kupiga vita ulevi wa hovyo hasa wa Shisha na dawa nyingine za kulevya ambazo zimewadhuru vijana wengi sana afya ya akili kiasi cha kuwa mzigo kwa Taifa. Kwani hawazalishi chochote katika kutoa mchango wao wa kiuchumi kwa taifa hili.

Wapo waliofanya mazuri huko nyuma na walifanikiwa kufanya kazi zao kwa ujasiri lakini wengi ilikuwa ni enzi ya utawala wa chama kimoja, yeye Makonda anayafanya haya katika enzi hizi za vyama vingi ambazo zimekumbwa na baadhi ya watu wasiokubali hata ukweli wa wazi kabisa.

Walichofundishwa wao ni kupinga chochote kile hata kama ni cha manufaa kwa taifa. Wapinzani na wanaharakati hawa ambao wengine ni wasomi, watu wa dini na wazee wa hekima lakini hawana lolote wanalolifanya kunadi maendeleo ya nchi hii zidi ya kila kukicha kuleta madudu ya kukwamisha juhudi za chama tawala na serikali yake kuwaletea wananchi wake maendeleo ya kweli na ya dhati.

Kitendo cha Makonda kufanya ziara ya nchi nzima kukagua utekelezaji wa Ilani ya CCM na kuona kero za wananchi na kuzitatua ni historia ya pekee kwa taifa hili. Si kwamba kitu hiki hakijawahi kufanywa huko nyuma. La hasha.

Kiliwahi kufanywa na viongozi kadhaa wakiwemo aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili, Ali Hassan Mwinyi na aliyewahi kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani na Naibu Waziri Mkuu, marehemu Augustine Lyatonga Mrema.

Lakini tofauti ya Makonda na hao watangulizi wake ni kwamba Rais mstaafu Mwinyi alisikiliza kero za wananchi kwa kwenda Ofisi ndogo za Chama Cha Mapinduzi (CCM) pale Mtaa wa Lumumba jijini Dar es Salaam huku marehemu Mrema alikuwa akifanyia kazi zake hizo za kusikiliza wananchi Wizarani kwake.

Mrema alikuwa akiwaita watuhumiwa hukohuko ofisini huku wengine akiwapa wiki moja kutatua makosa yao na hasa wale waliokuwa wakiwanyanyasa wake zao.

Pia kwenye awamu hii ya sita kuna nyakati jopo la mawaziri lilikuwa linatembelea mikoa mbalimbali kusikiliza kero za wananchi ambazo nyingi zilikuwa za migogoro ya ardhi ya kugombea mashamba, nyumba na kadhalika.

Makonda alipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam pia kuna baadhi ya kero alikuwa anazisikiliza pale ofisini kwake Ilala Boma, lakini sasa amejiongeza kwani ameamua kuwafuata huko huko waliko na kuwataka kusema kero zao za aina yoyote hadharani na yeye kutoa maamuzi ya papo kwa papo ambayo si ya kumwonea mtu wala kumpendelea.

Niseme tu hapa kwamba ziara hizi za Mwenezi Makonda ziwe endelevu ikiwezekana azifanye kila baada ya miezi mitatu.

Kwa nini nasema hivi? Ni kwa sababu binafsi nawajua Watanzania. Wengi wetu hufanya vitu kwa woga au kwa unafiki. Nakumbuka alipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam hili lilijitokeza wakati wa ziara yake moja ya Mabwepande wilayani Kinondoni.

Kuna kiongozi aliyekuwa akiwanyima maji ya kisima wananchi wa kule, lakini aliposikia Makonda anakwenda huko alitoa maji kwa wakazi wale. Kitendo kile kilikuwa cha woga na cha kizandiki wa hali ya juu hasa ukizingatia kisima kile kilichimbwa kupitia miradi ya serikali.

Kukomesha ubabaishaji kama ule ndiyo maana nashauri Makonda afanye ziara za aina hiyo kila baada ya miezi mitatu ili kuangalia yale anayoyaagiza kama yanatekelezwa. Hii ni namna nzuri ya kumsaidia Rais Samia katika kumaliza kero za wananchi.

Naamini kuwa Makonda kama ataendelea kuungwa mkono na wananchi hatoshindwa kufanya hivyo, kwani kikubwa kuliko vyote ni kwamba yeye bado ni kijana mwenye nguvu sambamba na kuwa na baraka zote kutoka kwenye chama chake na Rais Dk. Samia. Makonda ni mtoto wa mjini. Huwezi kudanganya kitu.

Kimsingi, Makonda hana sababu ya kuhofu chochote kile. Ni vyema ajue kuwa kila mtenda wema huwa hakosi maadui. Nimwambie tu kwamba haya anayoyafanya kwa ajili ya wananchi wanyonge, wananchi wanyonge ambao ndiye wengi pamoja na Mungu, muumba wa mbingu na ardhi wako pamoja na yeye.

*Kwa mawasiliano na mwandishi wa makala haya. 0784 122 020/ 0768 888 787.*

Demokrasia

# Hamjajua tu Samia ni mama wa demokrasia Tanzania?

Na Hamid Yassin

WIKI iliyopita, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan alilitaka Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) na vyombo vingine vya ulinzi na usalama kujiandaa katika kuhakikisha uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka huu na Uchaguzi Mkuu wa utakaofanyika mwakani zinafanyika kwa usalama na amani.

Hata hivyo, kumeibuka makundi ya watu yakitoa tafsiri upotofu juu ya kauli yake hiyo njema.

Baadhi ya wanaharakati, wanazuoni na wanasiasa wameanza kujenga hoja usiyo na mashiko juu ya kauli hiyo, eti kwamba kuna kitu kimejificha nyuma ya pazia la agizo hilo la Amiri Jeshi Mkuu, Dk. Samia!

Katika uchambuzi wao wamedai eti kauli ya Rais Samia kulitaka Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) na vyombo vingine vya dola kujiandaa kukabiliana na chochote wakati wa uchaguzi kuwa ni tishio kwa demokrasia.

Wakizungumza na Sauti ya Amerika (VoA) baadhi ya wanazuoni kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wamedai kauli hiyo inaweza kuleta mikanganyiko.

Aidha, wamedai kuwa suala la uchaguzi ni suala la kiraia na jeshi la ulini halipaswi kuingilia kwenye masuala ya chaguzi ili kuepusha kuleta wasiwasi miongoni mwa wananchi na wanasiasa.

Mhadhiri wa masuala ya siasa kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Richard Mbunda amedai kwamba kulitaka Jeshi la Wananchi kuingilia masuala ya uchaguzi inaonesha kuwa pengine uchaguzi unakuwa haufanyiki katika mazingira ya salama.

"Kumekuwa na malalamiko mengi kwamba vyombo hivi vimekuwa vinatumika kutengeneza matokeo kwa hiyo unapotoa kauli kama hizo unakuwa unajaribu kuthibitisha zile hisia za wananchi kwamba yawezekana uchaguzi haufanyiki katika mazingira ya uwanja sawa. Yawezekana kwamba kuna vyombo vinavyotumika ambavyo vilitakiwa visiingilie masuala ya uchaguzi," amedai Dk. Mbunda.

Wachambuzi hao wamezidi kudai kwamba eti JWTZ ina majukumu ya msingi ikiwemo kulinda katiba na uhuru wa

Inaendelea Uk. 15



Demokrasia

**Halafu hawa wachambuzi wanadhani Tanzania si Afrika, bara ambalo limeshuhudia chaguzi nyingi zikiwa sababu ya nchi kuingia kwenye machafuko kama kuna ulinzi legelege? Hawajui kwamba Tanzania iko Afrika ambako kila chaguzi zikikaribia baadhi ya wageni hupunguza kuja na wengine walioko kwenye nchi hizo kuamua kuondoka kusubiri uchaguzi upite.**

**Inatoka Uk. 14**

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ulinzi wa mipaka pamoja na kushirikiana na mamlaka za kiraia kutoa misaada ya kibinadamu na uokoaji wakati wa maafa, lakini kushiriki katika uchaguzi sio miongoni mwa majukumu yao.

**JESHI 'LILALE' WAKATI UCHAGUZI?**

Kwangu mimi hii ni hatari kwa wasomi wetu kutoa kauli kama hizi. Msomi huyu anakiri kwamba moja ya jukumu la Jeshi la Wananchi ni kulinda katiba ya nchi, tena anasema ni jukumu la msingi, sasa chaguzi za nchi si masuala ya kikatiba? Yaani watu wavuruge chaguzi halafu vyombo vyetu vya usalama vikae kimya tu!

Halafu hawa wachambuzi wanadhani Tanzania si Afrika, bara ambalo limeshuhudia chaguzi nyingi zikiwa sababu ya nchi kuingia kwenye machafuko kama kuna ulinzi legelege? Hawajui kwamba Tanzania iko Afrika ambako kila chaguzi zikikaribia baadhi ya wageni hupunguza kuja na wengine walioko kwenye nchi hizo kuamua kuondoka kusubiri uchaguzi upite.

Ni kweli, Tanzania imekuwa ikiendesha chaguzi zake kwa amani lakini hiyo haiwezi kuwa sababu ya kutolikumbusha jeshi lisijibweteke.

Mchambuzi huyu anakubali kwamba JWTZ inatakiwa pia kushirikiana na mamlaka za kiraia kwenye kutoa misaada ya kibinadamu na uokoaji, lakini hataki lishiriki kwenye shughuli za uchaguzi eti siyo majukumu yao!

**JESHI HALISIMAMII UCHAGUZI**

Kwani Dk. Samia ameliagiza Jeshi lisimamie uchaguzi? Hapana tusipotoshe, yeye amelitaka likae tayari kuhakikisha usalama unakuwepo wakati wote wa chaguzi zetu.

Inaeleweka kuwa, wanajeshi wetu hawaruhusiwi kugombea nafasi za kisiasa na kushiriki kwenye kampeni basi, lakini majukumu mengine ni ruksa, ikiwemo kushiriki kuchagua viongozi wanaowataka, yaani kupiga kura na kusimamia usalama wa nchi wakati wote ikiwemo nyakati za chaguzi.

Kama tunadai JWTZ kazi yake pekee ni kulinda mipaka yetu na raia wake, kwa nini tunakubali wanapokuja kutoa misaada ya kijamii yanapotokea maafa kama mafuriko na kujenga madaraja ya muda, lakini iwe nongwa kulinda usalama nyakati za chaguzi?

Mhadhiri mwingine msaidizi, Sabatho Nyamsenda wa Idara ya Sayansi ya Siasa na Utawala wa Umma kutoka Chuo hiki kikuu cha Dar es Salaam yeye aliiambia VOA kuwa, serikali inapaswa kuhakikisha. shughuli za kisiasa haziingiliani na masuala ya jeshi na kwamba iwapo chama cha siasa kitakiuka sheria ya vyama vya siasa basi kinapaswa kufutwa kwa mujibu wa sheria na sio kutegemea dola.

"Kuchukua hatua za kisheria na kikatiba za kuhakikisha kwamba shughuli za kisiasa zinabaki kuwa za kisiasa na kama vyama vya siasa havifanyi shughuli zao kwa mujibu wa sheria haikubaliki," alisema

Nyamsenda akiongeza; "Sheria iko wazi, vinatakiwa kuondolewa lakini kama vinafanya kazi kwa mujibu wa katiba na sheria basi ni vyema vikaachwa kufanya shughuli zao na ukatengenezwa uwanja ambao ni tambarare kati ya vyama vya siasa na chama tawala ili chama tawala kisitegemee dola kubaki madarakani."

**UPINZANI UNAMINYWA?**

Nani alimwambia msomi huyu kwamba vyama vya upinzani vinabinywa hivi sasa kutimiza majukumu yao kisiasa? Tusiishi kwa mazoea, yaani tuache kukariri tu, hizi zama za Mama demokrasia Tanzania Dk. Samia Suluhu Hassan, hakuna ubabaishaji.

Huu sasa ni mwaka wa 29 tangu mfumo wa siasa wa vyama vingi uanze rasmi hapa nchini, hivi kuna mwaka watu waliona kwenye chaguzi za amani na utulivu Jeshi letu la Wananchi likiingia mitaani kusimamia usalama?

Tuliopitia Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) tunajua tu kwamba kipindi cha uchaguzi lazima Jeshi lichukue tahadhari, kizungu wanaita 'standby' (kuwa na utayari) ili kama kuna wapuuzi wachache watataka kutumia mwanya huo kuvuruga amani washughulikiwe.

Hiki ndicho alichokuwa akikikumbusha Amiri Jeshi Mkuu ili vijana wake wasije wakajibweteka au kama vijana wanavyosema siku hizi; "wakachukulia poa." Msomi anaposhindwa kuelewa hili kiasi ananishangaza.

**ZANZIBAR ILIKIWAJE**

Uchaguzi wa mwaka 2000 kule Zanzibar ulikuwa na matukio ya uvunjifu wa amani kiasi damu za watu zilimwagika, na visasi viliendelea hadi mwaka 2001 yalipotokea mauaji na umwagaji wa damu mkubwa kiasi kwa mara ya kwanza taifa lilizalisha wakimbizi nje ya nchi!

Katika hali kama ile Jeshi la Wananchi linakaaje pembeni, lazima liingilie kati kudhibiti matukio kama yale ya vurugu na uvunjifu wa.amani.

Narudia kusema.Hiki ndicho Dk. Samia alichoagiza majeshi yetu yote yakae tayari kukabiliana na matukio kama hayo; lakini si kuweka mazingira.ya kukipendelea chama tawala kama hawa wanaharakati wanavyotafsiri.

Naye Mbwana Aliamutu, Mchambuzi wa siasa kutoka Morogoro alisema kauli ya Rais inaweza kuleta mitazamo tofauti kwa vyama vya upinzani na kuonesha kurudisha nyuma jitihada za demokrasia ya nchi na kwamba kauli hiyo inaonesha vitisho kwa vyama vya upinzani kuelekea chaguzi za serikali kuu na serikali za mitaa.

"Vyama vya upinzani vinaweza vikaitazama kauli hii kwamba ni kauli inayorudisha nyuma jitihada kubwa za demokrasia kwa nchi ya Tanzania na wanaweza wakaitazama pia kama kauli ya vitisho kuonyesha dira ya kuelekea kwenye uchaguzi kutakuwa na utumiaji wa dola na nguvu kwa maana ya vyombo vya ulinzi na usalama kuweza kulinda chama kilichopo madarakani."

**KIPINDI KISIWE CHA UPANDE MMOJA**

Kwa mtazamo wangu watayarishaji wa kipindi hicho hawakuwa 'feya'. Walitakiwa pia kuandaa wazungumzaji kutoka serikalini ili kutoa ufafanuzi juu ya kauli hiyo ya Dk. Samia na hivyo kuepusha utoaji wa tafsiri potofu ambazo ninaweza pia kuziita za kichochezi!

Kimsingi, huo ni mtazamo wao lakini sisi wasikilizaji wa kipindi tulitakiwa pia kusikia hoja pinzani za upande wa pili ili kila msikilizaji apime ni hoja gani anaona ni sahihi.

Hii inaweza pia kuonekana kana kwamba VOA walikuwa na ajenda yao ya kutafuta watu wa upande wanaotaka kwa sababu sikusikia wakisema kana kwamba wamewatafuta viongozi wa serikali wakakosa ushirikiano.

**UCHOKOZI AU UCHOCHEZI**

Huu ni kama uchochezi, kwa sababu hakuna sehemu Dk. Samia ametoa kauli ya kuviagiza hivi vyombo vya dola kuiwekea CCM na Serikali yake mazingira wezeshi ya kushinda chaguzi!

Amevitaka vihakikishe chaguzi zinafanyika kwa amani na utulivu jambo ambalo lina faida kwa vyama vyote vya siasa vikiwemo vile vya upinzani, yaani wafuasi na viongozi wao pia.

Labda niulize swali. Kuna mpinzani ambaye angependa kuona vurugu na uvunjifu wa amani unatokea kwenye uchaguzi?

Hivi hamjui kwamba kwa jinsi tunavyoenenda huku serikali ya CCM ukiendelea kutekeleza vizuri Ilani yake, upinzani unaweza kuwa mkali ndani ya chama hicho tawala kuliko hata nje ya chama katika baadhi ya maeneo.

Nyiye wachambuzi mnasemaje pale jina la mgombea fulani wa CCM litakapokatwa au kushindwa kupenya halafu, kwa mfano, yeye na kundi lake wakaanzisha vurugu? Hapo mnataka vyombo vya dola viwe vimejibweteka tu?

**NANI ANASIMAMIA UCHAGUZI**

Katika kuchambua mustakabali wa demokrasia hapa Tanzania na Afrika kwa ujumla, ni vyema kupambanua baina ya malengo ya mwisho na vyombo vya lazima vya kuyafikia. Italeta maana kwa taifa letu kupambanua baina ya haki za msingi na haki za vyombo vya utekelezaji.

Yaani Tume ya Taifa ya Uchaguzi ndiyo yenye mamlaka ya kusimamia chaguzi zetu na vyombo vya usalama vina jukumu la kuhakikisha chaguzi hizo zinafanyika katika hali ya utulivu na amani.

Haki ya kupiga kura, kwa mfano, ni haki ya utekelezaji iliyokusudiwa kutusaidia kufanikisha haki ya msingi ya Serikali kuwa na ridhaa ya wananchi.

Haki ya uhuru wa habari ni haki ya utekelezaji inayokusudiwa kutusaidia kufanikisha jamii iliyo wazi na uhuru wa kupata habari sahihi nyakati hizo za chaguzi.

**NCHI KUWA NA MAADUI**

Nchi kama yetu, nchi yenye amani na utulivu huku uchumi wetu ukizidi kuimarika haiwezi kukosa maadui wa ndani na wa nje.

Kulinganisha na mataifa yanayotuzunguka, Tanzania tumeendelea kuwa na utulivu na amani. Ni kutokana na utulivu huu, tumeendelea kuvutia wawekezaji na hata watalii. Yaani watu ambao wangeweza kwenda kuwekeza nchi nyingine wanavutuka kuja Tanzania kwa sababu ya amani na utulivu wetu tu!

Tumeendelea kuboresha barabara zetu, shule zetu hadi bandari na kumbuka ni eneo nyeti kwani kuna nchi tunashindana nazo kwenye biashara hizo.Hivyo lazima uwe macho na maeneo nyeti kama ya chaguzi ambayo watu wasioitakia mema nchi yetu wanaweza kuyatumia mwonekane na nyiye hamna amani!

Kumbuka Vijana Jazz Band waliwahi kuimba wimbo uitwao Mama Chichi wakasema maneno haya yanayofaa kuandikwa kwa wino wa dhahabu: "Kasoro za binadamu tangu enzi na enzi, kutopenda maendeleo ya mwingine..."

**SAMIA MAMA WA DEMOKRASIA**

Tunapokuwa tunamjadili mtu ni vyema tuangalie aina ya mtu huyo, tabia zake, hulka zake na matendo yake.

Samia tangu aingie madarakani, alikuja na 'R' zake nne ambazo zote anazifanyia kazi kwa vitendo. Hizi ni kifupisho cha maneno ya Kiingereza Reconciliation (Maridhiano), Resilience (Ustahimilivu), Reform (Mabadiliko) na Rebuilding (Kujenga upya).

Dk. Samia amerudisha mikutano ya hadhara, amefuta kesi kadhaa za washtakiwa wa kisiasa, ameridhia mijadala yenye mashiko na nchi yetu, kurudhia maoni na mabadiliko ya sheria za uchaguzi lakini kubwa amerudisha mazungumzo ya kisiasa mezani.

Mama amepanua wigo wa uhuru wa habari ikiwa ni pamoja na kufungulia magazeti yaliyokuwa yamefungiwa.

Lakini pia mmeona wiki iliyopita jinsi majeshi yetu yalivyolinda maandamano ya amani ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

Mtu anaweza kusema maandamano ni haki ya kikatiba, sawa; lakini si mpaka watawala wakubali. Wangekataa nani angetia mguu wake barabarani

Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe kwa mara ya kwanza alibeba hadi watoto wake wanne na kuandamana nao pamoja; Kwa nini alifanya hivyo? Jibu ni rahisi tu alikuwa na uhakika wa usalama wake na wanawe!

Hivi ndivyo Mama wa demokrasia hapa nchini Dk. Samia anataka iwe wakati wa chaguzi zetu za Serikali ya Mitaa mwaka huu na ule Mkuu mwakani. Yaani wananchi watoke majumbani mwao wakiwa na uhakika wa kupiga kura kwa amani na utulivu kama Mbowe na wenzake walivyoandamana na familia zao kwa amani na utulivu!

***Kwa mawasiliano na mwandishi wa makala haya; 0768 888 787/122 020.***



# Kurunzi

Na Dk. Reubeni Lumbagala | 0620 800 462

# 4R za Samia msingi wa maendeleo

UONGOZI bora ni nyenzo muhimu ya kufikia maendeleo. Ndiyo maana Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, enzi za uhai wake aliwahi kusema, ili nchi ipate maendeleo inahitaji kuwa na vitu vinne ambavyo ni watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora.

Vitu hivi vinne kwa pamoja vikitumika ipasavyo, vinakuwa nyenzo madhubuti ya kuchechemua maendeleo kwa ustawi wa maisha ya watu na nchi yao.

Rais wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan amedhirisha kwamba ni kiongozi bora ambaye anafanya juhudi kubwa kuhakikisha nchi yetu inapiga hatua za kimaendeleo kwa kuleta umoja na mshikamano nchini.

Kwa kuzingatia kuwa ujenzi wa taifa unahitaji mchango wa kila mwananchi bila kujali tofauti za kisiasa, dini, jinsi, ukanda, Rais Samia amekuwa akisisitiza na kuishi maneno yake ya kuhimiza umoja wa kitaifa ili kila mwananchi ashiriki kwa uhuru katika ujenzi wa nchi yake kupitia maarifa, mawazo, elimu na shughuli za kiuchumi anazofanya.

Moja ya falsafa aliyoiasisi Rais Samia katika ujenzi wa nchi yetu ni kuja na 'R' zipatazo nne (4R). Hizi ni kifupisho cha maneno ya Kiingereza Reconciliation (Maridhiano), Resilience (Ustahimilivu), Reform (Mabadiliko) na Rebuiding (Kujenga upya).

Maridhiano (Reconciliation) ni kitu muhimu katika ujenzi wa taifa ili kuwa na sauti moja. Rais Samia anaamini maridhiano na maelewano yanawezekana kwa kukaa pamoja na kujadiliana kwa njia ya mazungumzo na ya amani.

Palipo na maridhiano kuna maelewano, palipo na maelewano kuna amani na hivyo kuna kusonga mbele kimaendeleo. Maridhiano yanachagiza usuluhishi wa tofauti za kisiasa ili kushirikiana kwa pamoja kujenga Mama Tanzania.

Mathalani, Rais Samia ameshiriki kukaa meza moja na viongozi wa vyama vya upinzani ili kuwa na maridhiano yaliyolenga kutibu majeraha ya kisiasa na hivyo kuwa na mwanzo mwingine mzuri katika kujenga umoja wa kitaifa.

Kuongoza vyema ni pamoja kuwa mstahimilivu ukishinda majaribu mbalimbali kwani Waswahili wanasema mti wenye matunda ndio hurushiwa mawe na pia wanasema uongozi au ukubwa ni jalala. Kila mtu hutupa takataka zake hapo!

Kwa hiyo utaona ustahimilivu (Resilience) katika nchi utawezesha nchi kusonga mbele kimaendeleo. Uongozi wenye ustahimilivu utaweza kuvumilia changamoto na kukabiliana nazo ili kuzitafutia ufumbuzi wa kudumu kwa ustawi wa maendeleo ya wananchi wake.

Viongozi hawapaswi kuyumba wanapokumbana na changamoto bali wanapaswa kusimama kwenye nafasi zao na kushirikiana na wengine kuhakikisha changamoto zinapatiwa ufumbuzi wa kudumu ili wananchi wapate maendeleo.

Mabadiliko/Mageuzi (Reforms) hayaepukiki katika ujenzi wa nchi kwani kuleta maendeleo endelevu kunahusisha mageuzi.

Serikai ya Samia imeweka msukumo mkubwa katika kuleta mageuzi makubwa katika kila nyanja ikiwemo mageuzi ya sheria, sera na kanuni mbalimbali ili kuakisi mazingira ya wakati tulionao na hivyo kufikia azma ya kupiga hatua kimaendeleo.

Mageuzi yameonekana katika sera ya elimu, sheria za uchaguzi na sheria mbalimbali katika wizara tofautitofauti yakilenga kuongeza tija na maendeleo. Mkazo katika mageuzi au mabadiliko ya sheria ni kuongeza kasi ya maendeleo kwa kuondoa vikwazo vinavyokwamisha kufikia malengo na mipango ya serikali katika kuwatumikia wananchi wake.

Kujenga upya (Rebuiding) kumekuwa moja ya msisitizo mkubwa wa Rais Samia katika ujenzi wa nchi. Kazi kubwa za kimaendeleo zimefanyika katika awamu tano za watangulizi wa Rais Samia.

Kwa upande wake, Samia analo jukumu la kuacha alama katika nchi. Rais Samia anasisitiza umaliziwaji wa miradi ya maendeleo ya awamu zilizopita na kuja na miradi mipya ya maendeleo na ya kimkakati ili kupitia miradi hiyo, wananchi wapate maisha bora, ndiyo maana ya kaulimbiu yake ya "Kazi iendelee" kwani watangulizi wake wote wamekuwa na dhamira njema ya kujenga upya nchi.

Kujenga upya nchi kunahusisha kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi, kujenga miundombinu na uboreshwaji wa huduma za kijamii. Haya na mengine mengi mapya yanayofanyika chini ya uongozi mahiri wa Rais Samia yanatimiza mwekeleo wake wa kuijenga upya nchi yetu hasa katika nyanya ya kiuchumi na kijamii.

Januari 21, 2024, Rais Samia alishiriki ibada maalumu ya kumuingiza kazini Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Alex Malasusa, ibada iliyofanyika katika viwanja vya Kanisa Kuu la Azania Front, Dayosisi ya Mashariki na Pwani.

Katika ibada hiyo, Rais Samia alisema ili kuwe na amani na mshikamano wa kitaifa, serikali yake imekuja na falsafa ya 4R ambazo atazitumia katika uchaguzi wa serikali za mitaa pamoja na uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

"Baba Askofu Malasusa, umezungumzia umoja, amani na mshikamano wa kitaifa, kuhusu amani nakubaliana nawe kwa asilimia 100 kwamba tukiwa wamoja tutajenga taifa lenye nguvu. Katika uongozi huu, tumekuja na falsafa ya R4, Kiswahili chake ni maridhiano, mageuzi, ustahimilivu na kujenga upya taifa letu. Nizihusishe R4 na maneno yaliyosemwa kwenye kitabu cha Marko sura ya 3: 25 – Na nyumba ikifitinika juu ya nafsi yake, nyumba hiyo haiwezi kusimama" amesema Rais Samia.

Vilevile, Rais Samia alisisitiza kuwa 4R zitasaidia kukuza demokrasia nchini. "Si kila aliye kwenye mchakato wa demokrasia ni mwanademokrasia, wengine ni wanaharakati, kuna tofauti na haya mawili, tutaendelea kulinda misingi ya demokrasia hapa nchini kwetu inayowezesha demokrasia kushamiri zaidi," alisema Rais Samia.

Katika kuonesha kwamba Samia anayaishi maneno na ahadi zake, Jumatano iliyopita (Januari 24), Chama Kikuu cha Upinzani nchini (CHADEMA) kilifanya maandamano kushinikiza serikali kuondoa bungeni miswada mitatu ya mabadiliko ya sheria za uchaguzi na kuboresha katiba mpya, pamoja na mambo mengine.

Kwa lugha nyingine chama hicho kinataka serikali kufuata maoni ya chama hicho katika kuboresha miswada hiyo!

Wengi walidhani serikali ingezuia maandamano hayo ya amani lakini uongozi wa serikali ya Awamu ya Sita haukuzuia abadani maandamano hayo.

Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, pamoja na viongozi wengine wa chama hicho, Godbless Lema, Benson Kigaila na Joseph Mbilinyi waliongoza msafara wa waandamanaji hao waliokuwa wameshika bendera za chama hicho na mabango yenye jumbe mbalimbali.

Jeshi la polisi lilitoa kibali cha kuwaruhusu kufanya maandamano hayo na kuahidi kuyasimamia.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya mji wa Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alifika eneo la Buguruni mapema asubuhi na kuanza kuongoza misafara ya pikipiki na magari kabla ya maandamano hayo kuanza

Kwa ujumla, maridhiano, ustahimilivu, mageuzi/mabadiliko pamoja na kujenga upya ni nyenzo muhimu ya amani, demokrasia na maendeleo nchini.

Pamoja na dhamira njema aliyonayo Rais wetu ya kutaka kuona 4R zinatekelezwa ipasavyo, viongozi wa dhima ya kutoa ushirikiano ipasavyo ili kukamilisha azma aliyonayo Rais Samia ya kutaka kuona Tanzania yenye amani, upendo, mshikamano, demokrasia na maendeleo. Hii inawezekana kwa kuitendea haki falsafa ya 4R kwa vitendo.





Paul Mng'ong'o

## KLINIKI YA FIKRA

Simu: 0676055444 Email: mngongopaul@yahoo.com

# Misumari ya mahusiano - 4

WIKI iliyopita, tuliendelea na somo hili lenye makusudi ya kuimarisha mahusiano yetu. Mambo haya unaweza kuyachukulia kirahisi au kutoyapa uzito, lakini ukiyazingatia na kuamua kwa dhati kuyatekeleza, huleta uimara wa mahusiano, amani na kuwajengea furaha. Karibu tuendelee safu hii sehemu ya nne (4) kwa faida yako na ustawi wa jamii yetu.

**15. KUWA MSAADA (HELP)-** Hii ndiyo sababu kuu iliyomfanya mtu anayeitwa mwenzi kuumbwa. Kwa wasomaji wa maandiko ( Mwanzo 2:18).

Mungu hakufanya tu aina yoyote ya msaada kwa mwanadamu, alimfanya mtu mwenzake wa jinsia tofauti (Mwenzi) kuwa msaada.

Ukipata nafasi ya kuwa mwenzi wa mtu, jambo lako la kwanza si kumkosoa, bali ni kuainisha maeneo mahsusi ambayo huyo mtu anahitaji msaada wako. Baada ya kutambua, basi jaza nafasi hiyo kwa kuwa msaada wa karibu na mfanye afurahi wewe kuwa msaada wake. Maeneo ya msaada ni mengi kama vile msaada kwenye mambo ya nyumbani, msaada wa kikazi, msaada wa kihisia na kimahusiano, msaada wa kisaikolojia, msaada wa kijamii, msaada wa kimaisha, ukuaji wake, maendeleo, n.k.

Hakikisha unakuwa msaada hii inaleta maana kubwa sana ya nafasi yako kama mwenzi. Katika kutekeleza hili, tambua kuwa kuwa unatakiwa kufanya hivyo kwa tabasamu, si kwa kulalamika na kusononeka.

Changamoto ya hapa nipate mwenzi ambaye anajiona mkamilifu na kwamba kwake wewe si lolote zaidi ya tendo la ndoa tu. Hapa ndipo mahusiano yaanza kuwaka moto. Hitaji hili ni kubwa zaidi kwa mwanaume kuliko hata kwa mwanamke. Mwanaume anahitaji msaada zaidi.

**16. FURAHA NA UCHESHI (HUMOUR) -** Maisha ni magumu na yenye "stress". Kila mtu anataka mwenzi anayeweza kumsaidia kucheka na kufurahi bila kujali changamoto za maisha. Kicheko hufanya ndoa kuwa ya kumbukumbu zaidi. Moyo wenye furaha ni dawa (Mithali 17:22).

Pamoja na kuwa hitaji hili lipo kwa wote, lakini huwezi kuamini, ni kubwa sana kwa mwanamke kuliko unadhani. Sasa mwanaume huenda usiwe mwongozaji wa kuchekesha au hata kuwa mzuri kwa kuchekesha, lakini unapaswa kuwa na uwezo wa kumfanya mkeo (mwenzi wako), acheke. Ukifanya hivi matokeo yake utayaona. Hili linaweza kuwa hitaji kubwa kwa mwanamke kuliko hata fedha unazodhani zinamtosha.

**17. AKILI (INTELLIGENCE) -** Uzuri unaweza kukusaidia kuwavuta wanaume, lakini akili itakusaidia kuwadumisha. Mwanamume anapenda mwanamke anayeweza kumtia hamasa kwa akili na kushiriki mazungumzo yenye akili. Anahitaji kujua kwamba unaweza kushiriki katika mazungumzo kuanzia upishi na mitindo hadi siasa, michezo au biashara. Hivyo basi, ili uwe bora, amua kwa dhati kusoma vitabu, sikiliza habari na endelea kujifunza (Rejea Mithali 11:22). Ukiangalia utaona katika hili nimekwenda moja kwa moja kwa mwanamke sababu ni hitaji la muhimu sana la mwanaume na ni hitaji la msingi.

**18. UKARIBU / UNYOEFU (INTIMACY) -** Watu wengi (hususan wanawake), wanaishi na wageni. Ni kweli mnakula chakula pamoja, mnalala kitanda kimoja na kuishi nyumba moja na mwenzi wako, lakini ninyi ni wageni kila mmoja kwa mwenzie. Hampo karibu, mnaishi kama mtu na shangazi, hata mambo yenu mnayoyofanya ni kuingiliana tu, lakini hamna ukaribu. Mwenzi wako (hususan mwanamke), anataka utumie muda naye, anataka kuwa rafiki yako wa karibu, anataka kushiriki hofu zake kubwa na siri zake, anataka nawe umshirikishe mambo yako kwa kina aelewe.

Anataka kuwa karibu nawe na kuhisi unganiko la kimwili na kihisia nawe.

Mwenzi wako anahitaji zaidi Romantic time nawe. Hii ndiyo huleta "Intimacy" na utoshelevu wa kihisia (Contentment). Lakini wenzi wengi hawana ukaribu huu ndiyo maana hata kwenye maeneo ya msingi wanayotakiwa kufika kihisia, hawafiki pamoja.

**19. KUFURAHI NA KU - "ENJOY" (JOVIAL) -** Pamoja na kuwa wenzi wote wanahitaji kufurahia maisha au kwa lugha nyingine ku – enjoy, ni vizuri tujue kuwa wanaume wanapenda kufurahi. Pamoja na kuwa si watoto tena, lakini wao kwa wenzi wao ni kama watoto na wanapenda kucheza. Ndiyo maana wanapenda wanawake wanaowapata wawe wale wanaoweza kuwaelewa, kufurahi na kucheza pia. Ukiwa mke wake, kazi yako siyo kumzuia mwanaume kufurahi na marafiki zake, bali kufurahi pamoja naye. Usijaribu kumzuia kucheza michezo yake ya kompyuta, michezo ya simu au hata michezo ya kimwili, badala yake jifunze jinsi ya kucheza nao ili uweze kufurahi pamoja naye.

Wanawake wengine wanajikuta wanachofanya ni kuhakikisha tu mwanaume hapati madhara ila anamsaidia kupata furaha anayoitaka. Mfano, akijua mwanaume wake anapenda games, anamnunulia game, anapenda mpira ananunua au kufunga DSTV au Azam TV, kama anapenda kuangalia mpira na washikaji zake anaweza kupita "one-time" akamuagizia anachotaka akamwacha anafurahi.

Hii inamfanya mwanamke kuwa sehemu ya maisha ya mtu kuliko kugeuka kuwa mwanaharakati na mpinzani. Kwa kuingia ndani ya furaha yake, unaweza kupata nafasi nzuri kudhibiti kwa busara hali kama inazidi.

**Wework Consult - Your Partner in Growth.**

**Itaendelea wiki ijayo...**



> **Uzuri unaweza kukusaidia kuwavuta wanaume, lakini akili itakusaidia kuwadumisha. Mwanamume anapenda mwanamke anayeweza kumtia hamasa kwa akili na kushiriki mazungumzo yenye akili. Anahitaji kujua kwamba unaweza kushiriki katika mazungumzo kuanzia upishi na mitindo hadi siasa, michezo au biashara. Hivyo basi, ili uwe bora, amua kwa dhati kusoma vitabu, sikiliza habari na endelea kujifunza (Rejea Mithali 11:22). Ukiangalia utaona katika hili nimekwenda moja kwa moja kwa mwanamke sababu ni hitaji la muhimu sana la mwanaume na ni hitaji la msingi.**



Na Hamisi Kibari

Mtanzani wa kwanza kushinda Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu

# Niko tayari kwa kifo - 17

**Chris anachukua ushauri wa daktari kuficha kifo cha mkewe aliyemkimbiza hospitali baada ya kumshushia kipigo kikali, hali inayofanya atumie gharama kubwa kufanikisha hilo. Baada ya kufilisika, Joyce aliyemwehusha akili na kusababisha ampige mkewe na kusababisha mauti yake anamkataa Chris na kugeukia kwa mwanaume mwingine na kusababisha Chris afanye fujo kubwa ya kumpinga Joyce na huyo mpenzi wake mpya na kuanza kutafautwa na polisi. Kutooneka kwake kunaleta wasiwasi mwingine hadi dada yake, Mwalimu Misango kufikiria kutoa picha kwenye magazeti. Katika hatua nyingine jirani wa Chris alipokuwa akiishi na mkewe anamjulisha wasiwasi walio nao kwamba hawaamini kama mke wa Chris, Mama Kenny, ni mzima kwani toka wasikie Chris akimpiga vibaya hawajamtia machoni. Lakini jirani huyo, Maua anamweleza Mwalimu Misango kitu kingine cha kushangaza, kwamba Mama Kenny amekuwa akijitokeza mtaani kwao, tena mchana kweupe kama mzimu... Nini mwisho wa mkasa huu? Endelea.**

"Ameshaonekana pale mtaani mara mbili. Anakuja akiwa katika mtu mfano wa Mama Kenny na gari aina ya IST nyeusi. Bila shaka sisi tunaona ni gari lakini pengine hicho ni kitu kingine."

"Bado sikuelewi Maua!

"Siku ya kwanza, watu waliona gari ikisimama kwenye nyumba ya Baba Kenny ambayo imeuzwa. Ilikuwa ni wiki moja baada ya aliyeinunua kuanza kuikarabati. Kama hujaiona tangu imeanza kukarabatiwa leo ukioona Mwalimu utaipotea kwa jinsi ilivyopendeza. Watu waliona gari ikisimama upande wa pili wa barabara kisha akashuka mwanamke aliyekuwa amejitanda ushungi. Waliomwona wanasema alisimama akiiangalia ile nyumba akiwa ameegemea gari. Mwanangu aliyekuwa anapita kuja ndani, ni mmoja wa waliomwona. Mwanzo hakufikiria kama anaweza kuwa Mama Kenny kutokana na mavazi. Mtaani hatujawahi kumwona Mama Kenny akiwa amejitanda ushungi, amevaa kama Muislamu anayetaka kuingia msikitini kuswali. Yaani alivaa kama mimi nilivyo.

"Sasa walipokutanisha macho akagundua ni Mama Kenny. Akamsalimia, akaitikia kwa kubabaika na mara akageuka na kuingia kwenye gari harakaharaka na kuondoka kwa kasi," alisema Maua huku Mwalimu Misango akiwa amemtumbulia macho. Akaongoza kwamba majirani wawili wengine waliopita karibu na mahala alipokuwa amesimama Mama Kenny walimwona lakini wakishindwa kujua kama yule ni yeye au mtu mwingine kutokana na mavazi alivyokuwa amevaa,

"Maua, wewe unaamini habari kama hizo?"

"Si nimekudokeza kwamba mimi mwenyewe nilishuhudia na ndio nilikuwa ninakuja huko kusimulia ilivyokuwa."

"Ulishuhudia?!"

"Ndiyo... Mwanzo hata mimi sikuamini hizi habari mpaka niliposhuhudia kwa macho yangu ndipo nikaamua kukutafuta. Ilikuwa juzi majira ya alfajirippyaani ilikuwa ndio kumepambazuka. Nilikuwa naandaa wanangu kwenda shule. Sasa yule mkubwa aliyemwona siku ya kwanza ndio alikuwa ameanza safari ya kwenda shule na mara akarudi ndani ghafla baada ya kutoka nje. Akaniambia 'mama mama, ile gari nyeusi umekuja tena'. Nikamuuliza gari gani? Akasema ile anayokuja nayo Mama Kenny. Ikabidi na mimi nitoke nje. Nilipotoka nikamwona anafunga mlango wa hiyo iliyokuwa nyumba yake. Kama kawaida alikuwa amevaa janabibi la rangi ya damu ya mzee na mtandao wa njano. Alipogeuka na kukuta ninamwangalia akainamisha sura yake na harakaharaka akaingia kwenye gari na kuondoka. Nilimwita 'Mama Kenny' lakini hakuitikia."

"Humo kwenye gari kulikuwa na dereva?" Akahoji Mwalimu Misango.

"Hapana, alikuwa peke yake na ndiye aliyeendesha."

"Haiingii akilini," alisema Mwalimu Misango. Akaendelea. "Mimi naona huyo mwanamke mnayemsema ana wajihi tu unaofanana na wifi yangu Mama Kenny na ndio walionunua hiyo nyumba. Waswahili wanasema duniani wawili wawili. Tangu lini Mama Kenny akajua kuendesha gari. Tangu lini Mama Kenny akawa mtu wa kuvaa mabaibui. Na pia ndhani ilikuwa bado gizagiza hukumwona vyema.

"Inawezekana, lakini fahamu tumeishi na Mama Kenny takribani miaka 10 paletaani kiasi kwamba hata gizani unamtambua lakini juzi nilivyomwona kulikuwa kumepambazuka kabisa."

> **Maisha ya namna hii yana maana gani tena kwangu? Heri nikifie jela au nijiue. Kwanza mimi tayari ni mfungwa au marehemu anayetembea. Pengine ili kunikomoa aneshawaambia polisi kwamba nilimuua mke wangu na ndio maana polisi wananitafuta kwa udi na uvumba.**

"Mimi ninakushukuru kwa taarifa yako, lakini la muhimu ni kufanyia kazi hizo hisia kwamba huenda mdogo wangu alimuua mkewe kwa kipigo. Pia unasema watu wanahisi alikwenda kumtupa au kumzika Mama Kenny usiku huohuo. Haya yote yanapaswa yafahamike kwa polisi ili wayafanyie kazi."

"Huogopi mdogo wako kunyongwa kwa mauaji."

"Kama kweli alimuua mkewe, hatuwezi kumkingia kifua muuaji. Haki ya mhalifu ni kulipia alichokifanya. Majirani wenye taarifa isaidieni polisi badala ya kukaa kimya eti mnaogopa kutoa ushahidi. Huyo Mama Kenny angekuwa ndugu yako ungeogopa kutoa ushahidi."

"Mwalimu, wewe ni mwanamke shujaa sana. Nimekuelewa."

***

Chris akiwa amevaa kofia pana huku ameshika kitu mkononi alisimama gizani usiku, jirani na nyumba aliyopangishiwa Joyce na mpenzi wake mpya. "Siwezi kukubali. Yaani anifilisi, awe chanzo cha kifo cha mke wangu mpenzi Tausi, kisha amgawie mshenzi mwingine penzi huku akidhulumu duka langu. Siwezi kukubali. Ama zake ama zangu leo," alijisemea.Aliangalia saa yake na kuendelea kujiuliza, "Maisha ya namna hii yana maana gani tena kwangu? Heri nikifie jela au nijiue. Kwanza mimi tayari ni mfungwa au marehemu anayetembea. Pengine ili kunikomoa aneshawaambia polisi kwamba nilimuua mke wangu na ndio maana polisi wananitafuta kwa udi na uvumba."

Baada ya kupita nusu saa nyingine huku akiendelea kusubiri na kufukuza mbu, aliangalia tena saa yake: "Au leo hawarudi? Au nikawaangalie tena baa? No, ngoja nisubiri kidogo," alijisemea.

Katika kupelekeza kupitia kwa mmoja wa marafiki wa Joyce ambaye pia alisikitishwa na shoga yake kumtema Chris baada kuwa 'apeche alolo', aligundua kwamba ilikuwa haijawahi kutokea mpenzi wake mpya akalala nje kwa kuwa alikuwa pia na mke. Na ilikuwa ni nadra kwa mwanaume huyo kukaa baa na Joyce hadi usiku mwingi kama ilivyokuwa kwake.

Habari hizo zilimshangaza kidogo akikumbuka namna Joyce alivyokuwa akimng'ang'ania asiende kulala nyumbani kwa mke wake wakati penzi lao likiwa motomoto.Ingawa hakuwa anategemea kuona bado watu wakitembea usiku ule aliendelea kusimama mahala ambapo aliamini si rahisi mtu kumwona.

Baada ya kusimama takribani saa nzima na kuanza kuhisi uchovu wa kusimama muda mrefu aliamua kwenda kuketi kwenye kisiki cha mwembe eneo hilo la nje ya mji na ambalo kwa wakati huo lilikuwa linajengwa kwa kasi na wenye pesa zao.

Dakika chache baadaye huku akielekea kukata tamaa na kujiandaa kuondoka, Chris aliona gari dogo likija. Likasimama nje ya nyumba ambayo alipeleleza na kugundua kwamba ndipo alipokuwa akiishi Joyce akiwa amepangishwa na huyo bwana yake mpya, alimwona Joyce akishuka. Yule mwanaume aliyekuwa akiendesha lile gari naye akashuka. Wakakumbatiana kwa muda wakipigana busu kisha wakaachiana. Roho ikamuuma sana Chris. Kwa hakika alikuwa bado akimpenda sana Joyce ambaye sasa alijua hakuwa na mapenzi hata chembe juu yake isipokuwa pesa zake!

Aliamini pia hata kwa huyo mwanaume kinachopendwa ni pochi lake na si kingine.Akiwa sasa kasimama gizani, mahala ambako ilikuwa si rahisi kuonekana akamwona yule bwana anaelekea kupanda gari lake dogo.

Kuna wazo lilimjia la kumvamia yule bwana aliyemzidi kete lakini akasita. Kama kuna mtu alikuwa akimchukia zaidi duniani ni mwanaume huyo aliyemchukua mwanamke aliyekuwa akimpenda kupindukia.

Alimwombea kila baya. Alitamani kusikia usiku huo kapinduka na gari lake na kufariki dunia. Akamwona akiwasha gari na kuondoka.

Chris aliona kosa alilofanya mwanaume huyo. Alitakiwa kuhakikisha Joyce anaingia ndani na ndipo aondoke. Lakini kwa hali ilivyo wawili hawa hawakutarajia hatari yoyote katika eneo hilo tulivu hata kama muda ulikuwa umeenda sana. Saa saba kasorobo usiku. Kama ni tishio lake yeye Chris, bila shaka walijua wamesharipoti polisi ingawa hawakuwa na uhakika kama keshakamatwa ama la.

Hata yeye wakati akija kufanya mawindo hayo alikuwa anawaza namna ambavyo angefanikiwa kuingia ndani au kumfanya Joyce atoke nje lakini sasa aliona kazi yake ya kumvamia kabla hajaingia ndani ni nyepesi.

*Itaendelea*

# Zuma asimamishwa uanachama wa ANC

**JOHANNESBURG, Afrika Kusini**



CHAMA Tawala nchini Afrika Kusini cha African National Congress (ANC), kimeamua kumsimamisha kama mwanachama wake Rais wa zamani wa nchi hiyo, Jacob Zuma, tovuti za habari za ndani zimenukuu vyanzo vya ANC ambavyo havikutajwa majina.

Uamuzi huo ulichukuliwa na Bodi Kuu ya Uongozi ya ANC, Kamati Kuu ya Kitaifa kufuatia tangazo la Zuma mwezi uliopita kwamba atafanya kampeni kwa chama kipya, Umkhonto we Sizwe (MK), katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa baadaye mwaka huu, News24 na TimesLive zimeripoti.

Zuma alisema atasalia kuwa mwanachama wa ANC, lakini utakuwa usaliti kufanya kampeni kwa ANC ya Rais wa sasa, Cyril Ramaphosa.

Zuma amehutubia mikutano kadhaa ya Umkhonto we Sizwe, ambayo ina maana ya mkuki wa taifa na ni jina sawa na tawi la zamani la ANC.

Pia hutumia kifupisho sawa, MK. Hapo awali, ANC iliapa kuchukua hatua za kisheria kuzuia chama kipya kutumia jina hilo.

Zuma alijiuzulu kama kiongozi wa ANC baada ya kumalizika kwa mihula yake miwili mwaka wa 2018.

Mgombea aliyempendelea alipoteza kinyang'anyiro cha uongozi wa chama kwa kushindwa na Ramaphosa.

Kisha, Zuma alilazimika kujiuzulu kama Rais wa Afrika Kusini takriban miezi miwili baadaye kufuatia shinikizo kubwa kutoka ndani ya ANC.

Alifungwa mwaka 2021 kwa kudharau mahakama baada ya kukataa kutoa ushahidi mbele ya jopo lililokuwa likichunguza ufisadi wakati wa uongozi wake.

Kwa sasa anakabiliwa na mashitaka tofauti ya ufisadi kuhusu mkataba wa silaha ambao serikali ilijadiliana.

Alikuwa Kiongozi Mkuu wa ANC wakati huo, lakini si Rais. Mara kwa mara amekuwa akikanusha makosa yoyote, akisema alikuwa mwathirika wa uwindaji wa wachawi wa kisiasa. BBC.

## Makundi ya wapiganaji yajisalimisha DR Congo

**KINSHASA, DR Congo**

MWANDISHI wa AFP, amesema kundi lenye vijana wengi, liliwasili katika mji mkuu wa mkoa huo, Bunia, wakitumia magari kadhaa wakiwa wamevalia nguo za kiraia na bila ya silaha.

Msemaji wa kundi hilo linalojiita Zaire, Jean-Marie Ngadjole, alisema wamedhamiria na wako tayari kujiunga na mchakato wa amani na kushiriki katika mpango wa utangamano wa jamii utakaoongozwa na mamlaka za DRC.

Kundi hilo lilisema ni sehemu ya kundi la ulinzi lililoundwa mwaka wa 2019 kuyalinda maslahi ya jamii tano ambazo zimekuwa waathiriwa wa ukatili unaofanywa katika Mkoa wa Ituri karibu na mpaka na Uganda.

Kundi hilo linalojulikana kama `Zaire' linasema linawakilisha jamii za Hema, Mambisa, Alur, Akongo-Nyali na Ndo-Okebu na ni mpinzani wa Codeco, kundi la wapiganaji wanaosema dhamira yao ni kulinda kabila la Lendu dhidi ya Hema na washirika wao.

VOA.

> **Msemaji wa kundi hilo linalojiita Zaire, Jean-Marie Ngadjole, alisema wamedhamiria na wako tayari kujiunga na mchakato wa amani na kushiriki katika mpango wa utangamano wa jamii**

# Wanajeshi wa Marekani waliouawa shambulizi la Jordan watambuliwa

**WASHINGTON, Marekani**




SERIKALI ya Marekani imetoa majina ya wanajeshi watatu waliouawa katika shambulizi la ndege isiyo na rubani huko Jordan Jumapili iliyopita.

Wanajeshi hao ni Sgt William Jerome Rivers (46), Mtaalamu Kennedy Ladon Sanders (24) na Mtaalamu Breonna Alexsondria Moffett (23) waliouawa ndege isiyo na rubani iliposhambulia eneo lao la makazi.

Marekani imelaumu makundi yanayoungwa mkono na Iran kwa shambulio hilo na Pentagon na kusema limefuata nyayo za Hezbollah.

Pentagon pia ilisisitiza kuwa Marekani haitaki vita na Iran.

"Hatutafuti vita, lakini tutachukua hatua na kujibu mashambulizi dhidi ya vikosi vyetu," alisema Msemaji wa Pentagon, Sabrina Singh.

CBS News, mshirika wa BBC wa Marekani, alisema iliambiwa na afisa wa Marekani kwamba ndege isiyo na rubani iliyotumiwa katika shambulio hilo, inaonekana kuwa ya Iran.

Afisa huyo alisema ni aina ya ndege isiyo na rubani ya Shahed, droni ambayo Iran imekuwa ikitoa kwa Urusi.

Hata hivyo, Iran imekanusha shutuma za Marekani na Uingereza kwamba inaunga mkono makundi ya wanamgambo wanaolaumiwa kwa shambulizi hilo.

Pentagon ilisema wanajeshi watatu waliouawa Jumapili asubuhi walitoka katika kitengo cha wanajeshi wa akiba kilichopo Fort Moore, katika Jimbo la Georgia.

Luteni Jenerali Jody Daniels, Mkuu wa Hifadhi ya Jeshi na Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Akiba ya Marekani, alitoa pongezi kwa wanajeshi waliouawa.

"Kwa niaba ya Jeshi la Akiba, ninashiriki katika majonzi waliyonayo marafiki, familia na wapendwa wao. Utumishi na kujitolea kwao, havitasahaulika na tumejitolea kusaidia wale walioachwa nyuma kutokana na mkasa huu," alisema Jenerali Daniels.

Shambulio hilo la ndege zisizo na rubani lilifanyika Rukban Kaskazini-Mashariki mwa Jordan, karibu na mpaka wa Syria. Kituo hicho kilitajwa baadaye na maafisa wa Marekani kama Tower 22. BBC.

# Nigeria yakosoa nchi zilizojiondoa Ecowas

**ABUJA, Nigeria**

NIGERIA imesema kwamba viongozi wa kijeshi wasiochaguliwa na raia wa Niger, Mali na Burkina Faso, wamewasaliti watu wao, kufuatia uamuzi wa pamoja wa kujiondoa kwenye Shirika la Kiuchumi la Mataifa ya Afrika Magharibi (Ecowas).

Kwa mujibu wa Shirika la Habari la Reuters, Nigeria ambayo ni Mwenyekiti wa sasa wa Ecowas, imezungumza kwa mara ya kwanza baada ya mataifa hayo kutangaza Jumapili iliyopita kwamba yamejiondoa kwenye shirika hilo, ambalo limekuwepo kwa karibu miaka 50.

Wizara ya Mambo ya Kigeni ya Nigeria kupitia taarifa imesema kwamba wale wanaokusudia kujiondoa kwenye Ecowas, hawafanyi hivyo kwa nia njema.

"Badala yake, viongozi ambao hawajachaguliwa, wameamua kuhujumu haki ya wananchi ya uhuru wa kutembea, wa kufanya biashara, pamoja na uhuru wa kuchagua viongozi wao."

Hadi sasa, Ecowas haijatoa taarifa yoyote kufutia tangazo la kujiondoa kwa mataifa hayo. Hata hivyo, Nigeria imeongeza kwamba ipo tayari kushauriana na mataifa yote matatu kuhusu suala hilo.

VOA.



# Makocha waliowahi kukipiga AFCON





**Na Valensi Mbaga**

KATIKA nyanja ya michezo, kuna jambo la kipekee na la kustaajabisha ambapo wachezaji, baada ya kujitolea maisha yao kwa timu, hubadilika na kwenda katika nafasi ya ukocha wa timu hiyo hiyo. Safari hii ya kuvutia inaonyesha dhamira na uelewa wa kina, na utaalamu usio na kifani walio nao watu hawa kwa mataifa yao.

Tunapoingia katika ulimwengu wa wachezaji waliogeuzwa makocha, tunagundua simulizi za ajabu shauku, uongozi na uhusiano wa kudumu kati ya timu na mchezaji wake wa zamani. Wafuatao wamefanya makubwa wakiwa kama wachezaji na makocha kwa timu zao za kitaifa.

**1: Aliou Cissé (Senegal)**

Kocha wa Senegal Aliou Cissé ni mchezaji wa zamani wa kimataifa wa Senegal ambaye aliwakilisha vyema "Simba wa Teranga." Akijulikana kwa ukali wake wa ulinzi, alicheza jukumu muhimu katika safu ya ulinzi ya Senegal kwa miaka mingi. Aliou Cissé ameshiriki Kombe la Mataifa ya Afrika AFCON kama mchezaji na kocha. Mshindi wa fainali mwaka 2002 dhidi ya Cameroon nchini Mali kama mchezaji, hatimaye alishinda taji kama kocha mwaka 2021.

Akiwa amechezea vilabu kadhaa vya Ufaransa na Kiingereza, Aliou Cissé alimaliza maisha yake ya uchezaji mnamo 2009 kabla ya kuhamia ukocha. Mnamo 2012, alikua kocha msaidizi wa timu ya Senegal ya chini ya miaka -23, baadaye akawa kocha mkuu wa kitengo hicho hadi 2015.

Ilikuwa mwaka huo ambapo aliteuliwa kuwa kocha mkuu wa timu ya taifa ya Senegal. Mnamo Februari 2022, aliweka historia kwa kuipa Senegal taji lake la kwanza kabisa la AFCON . matumaini ya kuhifadhi taji hilo mwaka huu nchini Ivory Coast, yametokomea baada ya kutupwa nje ya michuano hii dhidi ya wenyeji Ivory coast.

**2: Rigobert Song (Cameroon)**

Timu ya Cameroon ni mojawapo ya timu zinazopendwa sana na wamekusanya mataji matano mpaka sasa.Timu hii inaongozwa na Rigobert Song, ambaye tayari ameng'ara kama mchezaji na nahodha wa timu hiyo kabla ya kuhamia kwenye ukocha.

>>Inaendelea uk. 21





# Makocha waliowahi kukipiga AFCON

>>Inatoka uk. 20

Alishinda AFCON mwaka 2000 na 2002 akiwa na nchi yake na baadae akapata nafasi yake ya kwanza ya ukocha katika timu hiyo. Katika maisha yake ya uchezaji, kocha huyo mwenye umri wa miaka 47 aliwakilisha vilabu kadhaa vya Ufaransa, Kiingereza na Kituruki.

Muda mfupi baada ya kuteuliwa kuwa mkuu wa Indomitable Lions, Rigobert Song alifanikiwa kufuzu Kombe la Dunia la FIFA lililopita nchini Qatar, na kuiondoa Algeria katika mchujo.

### 3: Kaba Diawara : Guinea

Timu ya taifa ya kandanda ya Guinea inaongozwa na Kaba Diawara, ambaye awali aliiwakilisha timu ya Ufaransa ya U-21 kabla ya kujiunga na nchi yake ya asili, akishiriki mara kadhaa katika Kombe la Mataifa ya Afrika akiwa mchezaji. Akiwa kwenye usukani anashiriki AFCON yake ya pili baada ya toleo la 2021 nchini Cameroon, akipania kuweka jina lake katika historia.

Akiwa mchezaji, Kaba Diawara alikipiga katika klabu mbalimbali za Ufaransa na Uingereza, zikiwemo Paris Saint-Germain, Olympique de Marseille, Arsenal, na West Ham. Alicheza pia Uturuki kabla ya kumaliza maisha yake ya uchezaji mwaka 2009.

Kaba Diawara amekuwa akiiongoza timu ya Guinea tangu Oktoba 2021. Kombe la Mataifa ya Afrika la mwisho nchini Cameroon lilikuwa uzoefu wake wa kwanza muhimu kama mkufunzi wa kandanda.

### 4: Juan Micha: Equatorial Guinea

Akiwa amethibitishwa kuwa kocha mkuu wa Equatorial Guinea Machi 2021 baada ya muda wa miezi mitano, Juan Obiang Micha ameiongoza Nzalang Nacional kwenye AFCON kwa toleo la pili mfululizo. Mwaka 2021 nchini cameroon, alifanikiwa pamoja na timu yake kufika robo fainali baada ya kuiondoa Mali katika hatua ya 16 na kuishinda Algeria katika hatua ya makundi.

Akiwa na umri wa miaka 48, Juan Michá Obiang Bicogo ni mwanasoka wa zamani wa Equatorial -Guinea ambaye aliichezea nchi yake mwishoni mwa miaka ya 1990 na mwanzoni mwa 2000.

Alianza taaluma yake ya ukocha katika klabu ya Fuenlabrada ya Uhispania kabla ya kujiunga na timu ya taifa ya wanawake ya Equatorial Guinea kama kocha msaidizi kuanzia 2012 hadi 2014. Timu za U17 na U20, pamoja na Deportivo Unidad, klabu iliyoko Malabo.

### 5: Baciro Cande: Guinea-Bissau

Baciro Cande amekuwa akiinoa timu ya taifa ya Guinea-Bissau tangu 2016. Mwaka huu nchini Côte d'Ivoire, aLIiongoza nchi yake katika michuano yake ya nne ya Kombe la Mataifa ya Afrika. Beki wa zamani wa Guinea Bissau pia alichezea Estrela de Amadora na Amara nchini Ureno kabla ya kuanza kazi ya ukocha.

Hii inakuwa nafasi yake ya pili katika usukani wa Djurtus baada ya uongozi wake wa awali kati ya 2001 na 2009. Wakati huo huo, pia aliifundisha Sporting Clube de Bissau (2009-2016), akiwaongoza kutwaa taji la ligi mwaka wa 2010. Mnamo 2023, bila shaka aliifundisha Sporting Clube de Bissau (2009-2016).








# Senegal watema Kombe

**ABIDJAN, Ivory Coast**

ULE Msemo wa mjinga ukiwa unakwenda wakati wa kurudi unajua njia umedhirika katika michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika baada ya Ivory Coast kukataa kufungwa mara ya pili na Senegal.

Pambano hilo liloisha kwa mikwaju ya penalti lilikuwa na Matukio mengi yalionyesha ubabe wa Soka Afrika.

Senegal waliokuwa wa kwanza kupata bao mapema zaidi ilionekana kama waliwafanya wenyeji ngazi.

Lakini kitendo cha nahodha Sadio Mane kucheza rafu mbaya katika kipindi cha kwanza bado linazunguka mitandaoni ikielezwa kuwa Ile kadi nyekundu ya moja kwa moja kwa kuwa alikuwa na kusudi la kumuumiza mwenzake.

Dakika 120 hazikutosha kuamua mshindi mpaka kufikia hatua ya matuta na Ivory Coast kuibuka kidedea.

Senegel walifanikiwa kupata nne huku wenyeji wakitumbukiza Tano.

Awali ilionekana mzani Unalalia Senegal lakini wenyeji walikuwa wakikumbuka vurugu zilizoibuka waliposhindwa kufuzu kwa hatua hiyo hadi kusubiri kapu la best looser.




# Arsenal haijasili mwezi huu

**LONDON. England**

KOCHA wa klabu ya Arsenal Mikel Arteta (41) amethibitisha kuwa hakuna usajili utakaofanyika katika dirisha dogo kwenye kikosi chake kwa mwezi huu january.

“Kutokana na kukosa mchezaji stahiki katika dirisha hili, imetupelekea kutofanya usajili wowote kwenye kikosi. chetu

“Najua tumekuwa hatuna kikosi kipana zaidi lakini kwa dirisha hili hatujaona mchezaji ambaye atakuwa bora zaidi wa kuweza kuja kuziba mapengo ya baadhi ya sehemu zenye uhitaji wa maboresho” alisema Arteta.



## Asia Cup:
# Qatar yaingoa Palestina



**DOHA, Qatae**

TIMU ya Taifa ya Qatar imeingia robo fainali ya michuano ya Kombe la Asia.

Qatar ilieponea chupu chupu kuondolewa baada ya kugeuza kibao na kuifunga Palestina mabao 2-1.

Pamoja na kuondolewa Palestina waliwapeleka pita mabingwa hao watetezi kwa muda wote wa mchezo.

Mashabiki wa Soka walionekana kuelewa Palestina katika michuano hiyo mkubwa.

# Conte huyo AC Milan

**MILAN, Italia**

KOCHA ha Antonio Conte (54) raia wa Italia inaelezwa kuwa amefikia makubaliano na AC Milan ili kuwa kocha mkuu wa klabu hiyo.

Conte ambaye kwasasa ni kocha huru tangu afutwe kazi na Tottenham Hotspurs ya Uingereza katikati ya msimu uliopita, anatajwa kujiunga na klabu ya AC Milan kwa msimu ujao 2024/2025.



# Cape Verde yaweka historia

**ABIDJAN, Ivory Coast**

CAPE Verde imeweka historia kwa kushinda mechi ya kwanza ya hatua ya mtoano ya AFCON kufuatia ushindi wa 1-0 dhidi Mauritania katika dimba la Félix Houphouët-Boigny mjini Abidjan.

Mauritania. Bao pakee la mchezo huo lilifungwa jioni kabisa katika 88 na Ryan Mendes.

Cape Verde imetangulia robo fainali kumsubiri mshindi kati ya Morocco dhidi ya Afrika Kusini.



# Nigeria katika kashfa ya dawa



**ABIDJAN, Ivory Coast**

KIKOSI cha timu ya Taifa ya Nigeria kimekumbwa na kashfa ya matumizi ya wachezaji wake kutumia dawa za kuongeza nguvu.

Zaidi ya wachezaji watatu wa kikosi hicho akiwemo Victor Osimhen watafanyiwa vipimo vya Afya baada ya kuhisiwa kuwa walitumia dawa za kuongeza Nguvu.

Wachezaji hao wameponzwa na mechi ya timu yao dhidi ya Cameroon.

Nigeria walisonga mbele kwa kuifumua Cameroon mabao 2-0.



## Kona ya Urembo

Na Hidaya Machuppa Simu: +255 765 828 219

# Vifaa vya kujiweka bomba






**Je, ni vifaa gani vyako vya kupendwa zaidi ili kuonekana kwenye mtindo zaidi?**

Kuangalia mtindo zaidi sio lazima kuvaa nguo za gharama kubwa au kufuata mitindo ya hivi karibuni.Inaweza kuwa rahisi kama kuongeza kitambaa au kurusha miwani ya jua. Mara nyingi, kuwa mtindo ni zaidi juu ya kujiamini na mtazamo kuliko kufahamu dhana changamano za mitindo. Jua ni nini lazima kiwe na vifaa unahitaji katika WARDROBE yako ambayo itachukua sura yako kwa kiwango kinachofuata.

### Miwani ya jua

Ikiwa utavaa nguo na unahisi kana kwamba inakosa kitu, inaweza kuwa miwani ya jua. Miwani ya jua inaweza



kubadilisha mara moja mwonekano wako na kuupa upekee na tabia. Miwani ya jua huvaliwa na icons za mtindo, watendaji na watu wengine wengi mashuhuri kwa sababu nzuri .Silhouettes za kawaida hazitokani na mtindo na zitafanya watu wengi waonekane maridadi na wa ajabu huku wakiweka macho yao bila miale ya UV. Katika mazingira ya kawaida, kama vile ukiwa ufukweni, unaweza kuchagua mitindo ya kuvutia zaidi na ya kisasa, ilhali katika hafla rasmi, unaweza kutafuta mwonekano wa kisasa na usio na wakati.

### Kofia

Mitindo inahusu kutoa taarifa na hakuna nyongeza nyingine inayoweza kutoa maelezo ya mtindo kama kofia. Kila mwanamume au mwanamke mwenye mtindo ana kofia mahali fulani kwenye vyumba vyao. Chaguo la kofia linaweza kujieleza kwa nguvu wewe ni nani na ikiwa ni ya maridadi au ya kawaida, inaweza kukufanya uonekane kutoka kwa umati.Kila mtu anapaswa kuwa na angalau wakati mmoja wa kofia maishani na mtindo wa hivi punde unaoonekana kwenye barabara za ndege mwaka huu ni sasisho kuhusu bereti ya kawaida.Kofia inaweza kuwa njia inayoonekana zaidi ya kufanya hisia na kuchukua mtindo wako wa kibinafsi kwenye ngazi inayofuata. Weka vito vyako

na silhouette ya vazi lako kwa urahisi ili kuvutia vazi lako maridadi.



### Mkanda

Kuongeza mkanda kwenye vazi kunaweza kuibadilisha kuwa kamili. Inaweza pia kuleta usawa kwa kuangalia ambayo inaweza kufanya kazi bila hiyo. Kuvaa sweta ndefu au vichwa vilivyolegea kunaweza kutumia ukanda ili kufafanua kiuno chako na kukifanya kionekane kidogo. Unaweza pia kuchagua mshipi unaoimarisha mtindo wako, kama vile wenye vijiti vya mwonekano wa kuvutia au wenye vito ikiwa ungependa kutambulisha mng'aro.


Mikanda ya elastic ina uwezo wa kubadilika kwani unaweza kuivaa juu au chini chini. Kuchagua mikanda nyeusi au kahawia inamaanisha kuwa unaweza kuivaa ukiwa na mavazi mengi tofauti mwaka mzima.Kuongeza mkanda kwenye vazi kunaweza kuibadilisha kuwa kamili. Inaweza pia kuleta usawa kwa kuangalia ambayo inaweza kufanya kazi bila hiyo. Kuvaa sweta ndefu au vichwa vilivyolegea kunaweza kutumia ukanda ili kufafanua kiuno chako na kukifanya kionekane kidogo. Unaweza pia kuchagua mshipi unaoimarisha mtindo wako, kama vile wenye vijiti vya mwonekano wa kuvutia au wenye vito ikiwa ungependa kutambulisha mng'aro.

### Vitambaa

Unaweza kutumia skafu kwa njia nyingi tofauti na nyongeza hii yenye matumizi mengi inaweza kuongeza ustaarabu kwa vazi lolote. Wanakuja katika rangi nyingi tofauti, textures, na mitindo. Kuongeza pop ya rangi kwenye sehemu ya juu ni rahisi kwa scarf ya rangi. Unaweza kucheza na rangi ya "katika" ya msimu kwa kutumia scarf na kuna njia nyingi za ubunifu za kufunga na kufunika.

### Viatu vya Msimu

Viatu ni nyongeza muhimu ya mtindo na inapaswa kuwa kivutio kikuu badala ya kufikiria baadaye. Jozi ya viatu inaweza kusema mengi kuhusu wewe na kuathiri hisia ya kwanza mtu anayo juu yako. Je, unapendelea kisigino kikubwa cha chunky au stiletto nyembamba? Labda baadhi ya kujaa kivitendo maridadi? Au jozi nzuri ya viatu vya kukupeleka karibu na mji kwa starehe?Na usisahau umuhimu wa mtindo wa jozi kubwa ya buti. Viatu vya juu vya kisigino na kanzu ya mfereji ni mtindo wa kuanguka / majira ya baridi, wakati buti zinazopanda, buti za mguu na buti za juu za paja ni lazima katika hali ya hewa ya baridi na inaweza kuunganishwa na skirt au mavazi ili kuonyesha gams yako.



> Mikufu ni msingi wa mtindo kwa kila ikoni ya mtindo. Kuweka minyororo mingi juu ya kila mmoja huunda mwonekano wa pande nyingi. Kutumia urefu tofauti kunaweza kuunda udanganyifu wa shingo ndefu na inaonekana nzuri.



### Mikufu

Mikufu ni msingi wa mtindo kwa kila ikoni ya mtindo. Kuweka minyororo mingi juu ya kila mmoja huunda mwonekano wa pande nyingi. Kutumia urefu tofauti kunaweza kuunda udanganyifu wa shingo ndefu na inaonekana nzuri na neckline ya chini.

Je! unataka mwonekano wa kisasa zaidi? Vito vya lulu havikosi mtindo na kuna njia nyingi ambazo unaweza kuziongeza kwenye mavazi yako - vaa kwenye nywele zako, kwenye kifundo cha mguu wako, au zaidi ya jadi kwa namna ya pete au shanga. Kwa mwonekano wa ujasiri, jaribu kutoa tamko kwa mkufu mmoja wa kushangaza au pete za taarifa.

### Mkoba wa Stylish

Nguo haijakamilika bila mkoba mzuri. Mikoba katika nyenzo tofauti na textures inaweza kuongeza ngazi nyingine kwa kuangalia yako na ni njia nyingine ya kueleza mtindo wako binafsi.

Fikiria mkoba wa ngozi, suede, mianzi, turubai, manyoya - chochote kinachoonyesha mtindo wako wa kibinafsi!

Leo yetu ndiyo kesho yetu

Uelekeo Spoti

| Jumatano Januari 31 - Februari 06, 2024 |

# Avuna bilioni kwa Benchi Mamelod

**CAPETOWN, Afrika Kusini**



MCHEZAJI Gift Motupa ametajirika kwa kukaa benchi kwa takribani msimu mzima wa Ligi Kuu ya Afrika Kusini akiwa na timu ya Mamelodi Sundowns.

Gift alikuwa akilipwa mshahara takribani milioni 120 kwa mwezi.

Klabu ya Mamelodi ilitangaza kuachana na nyota huyo kutokana na kutoridhishwa na kiwango chake kilichafanya avune pesa nyingi bila kuzitumikia.

Wakati Mamelodi wakitangaza kumtema, Gift alinunua timu inayoshiriki daraja la pili ya Seshengo Kings na kuibadili Jina kuwa Thogoaneng FC.

# Simba yaitega TFF



**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Bunge likielezwa kuwa timu za Bara zina uwezo wa kucheza Zanzibar kwenye Ligi Kuu, kanuni za michuano hiyo zinapinga.

Katika kikao kilichopita liliulizwa swali na mmoja wa wabunge kwamba kwanini timu za Bara haziutumii Uwanja wa Aman au Gombani Pemba katika michuano ya Ligi Kuu.

Naibu Waziri wa Sanaa, Utamaduni na Michezo, Hamis Mwinjuma alisema ruksa kwa timu za Bara kutumia uwanja wowote ndani ya Tanzania ikiwemo timu Zinazoshiriki Ligi Kuu.

Katika jibu hilo Mwinjuma alifafanua pia kuwa michuano ya Ligi Kuu ya Muungano inatarajiwa kurejea muda si mrefu kwa kuwa Kamati inayoshughulikia inakamkljsha Mchalato.

Kutokana na jibu hilo Simba waliamua kusafiria nyota hiyo na kuomba kutumia Uwanja wa Aman katika mechi zao za Ligi baada ya Uwanja wa Taifa kufungwa.

Hadi kufikia jana Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), haljjatoa majibu huku mechi ya Simba na Azam ikielezwa uwanja utathibitishwa baadae.

Lakini kanuni ya 9:4 ya ligi hiyo inasema mechi za Ligi Kuu zitachezwa katika viwanja vilivyopo Tanzania Bara pekee.

Hatua hiyo inaleta mgongano baina ya Kauli ya Waziri na TFF, huku ikielezwa Simba wameendelea kusisitiza kucheza Zanzibar.

"Simba wametuandikia barua ya kuomba kutumia uwanja mpya wa Amani kwa muda mpaka pale uwanja wa Uhuru na Uwanja wa Benjamini Mkapa utakapokuwa umerudi... utakapokuwa umeruhusiwa kuendelea na michezo yetu ya ligi.

"Kwahiyo tumepokea hiyo barua tunaendelea kuichakata, pale ambapo itakapokuwa tayari basi tutawafahamisha Simba na pia tutaufahamisha umma wa Watanzania maamuzi gani ambayo yamechukuliwa," alisema Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Almasi Kasongo.

# ... Wamalizana na Chama

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA sintofahamu ya muda mrefu kati ya klabu ya Simba na nyota wa Zambia Cletous Chama, suala hilo limefika mwisho.

Chama alisimamishwa siku chache kabla ligi haijasimama kupisha michuano ya Kimataifa na usajili kwa madai ya utovu wa nidhamu.

Mbali na Chama, Simba ilimsimamisha pia Nassor Kapama.

Kapama baadae aliondoka Simba na kutafuta changamoto nyingine nje ya klabu hiyo akiacha Chama akipambana na hali yake.

Uongozi wa Simba umeamua kumsamehe kiungo huyo kutokana na makosa ya yaliyokuwa yakimkabili.

Chama atajiunga na wenzie kambini kwa ajili ya michezo ya mzunguuko wa pili wa ligi pamoja na maandalizi ya mchezo wa CAFCL dhidi ya Asec Mimosas utakaochezwa nchini lvory Coast.

Chama atakuwepo kwenye michezo miwili ya ugenini ya viporo Simba SC dhidi ya Mashujaa FC na Tabora United.




# Sasa watanitambua

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kupata shavu la kurejea Umangani, Simon Msuva amepanga kujenga himaya yake huko.

Nyota aliyeifungia Tanzania bao pekee katika michuano ya Mataifa ya Afrika inayoendelea nchini Ivory Coast alisema anataka kufungua mtambo wa mabao huko Saudi Arabia.

Msuva aliyepata kuichezea timu ya Al-Qadsiah kwa msimu mmoja sasa amesajiliwa na Al Najma inayoshiriki kuu nchini humo.

"Nataka nifunge kule mpaka wanitambue, nina uzoefu na ligi yao si ligi nyepesi kama watu wanavyosema.

"Lengo langu jingine kucheza kwa muda mrefu zaidi kule, awali nilitamani iwe hiyo lakini baada ya Uongozi kubadilika kila kitu kilibadilika na kulazimika kuondoka," alisema.

Msuva ambaye mkataba wake na JS Kabylie ulivunjika alikuwa akitajwa kujiunga na Yanga dirisha dogo lakini mwenyewe alipinga kurudi Tanzania kwa sasa.

Mpaka sasa Msuva ameifikia rekodi ya pacha wake Mbwana Samatta kwa mabao katika timu ya Taifa wakifungwa mabao 22 kila mmoja.

"Lakini kwa sasa nimejiandaa kuhakikisha malengo yangu yanatimia. Kikubwa sio ligi nyepesi hivyo jambo la msingi ni kupambana ili kuweza kuisadia timu yangu," alisema.



## MATOKEO AFCON 2023 RAUNDI YA 16

**Angola 3-0 Namibia**
**Nigeria 2-0 Cameroon**
**Equatorial Guinea 0-1 Guinea**
**Misri 1-1 DRC (DRC 8-7 Misri kwa penalti)**
**Cape Verde 1-0 Mauritania**
**Senegal 1-1 Ivory Coast**
**(Ivory Coast 5 Senegal 4 penalti)**

## ROBO FAINALI

**Nigeria vs Angola**
**Guinea vs DRC**